# Nipashe
MWANGA WA JAMII

Ijumaa Septemba 25, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580349

www.ippmedia.com

itter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US






RC Ndikilo akagua uwekezaji mabilioni viwanda vya Kibaha

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

TARI: Zabibu zetu 'zimefunika' duniani

Choroko yalimwa kisasa, yatwaa chati kupendwa, zao la biashara

UKURASA 11

## CCM yataja mikakati 6 kukabiliana na majanga

UKURASA 2

# Msajili, upinzani wazidi kuvutana

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MATATANI MADAI KUBAKA MWANAFUNZI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa nchini (TAKUKURU), Wilaya ya Ikungi...

UKURASA WA 5

**ACT YATAMBA KUNYAKUA MAJIMBO YOTE TUNDURU**

CHAMA cha ACT-Wazalendo wilayani hapa kimetamba kupata ushindi wa kishindo...


## Mwanafunzi atuhumiwa kumkata mapanga mwalimu

UKURASA 4



Mrisho Gambo
**Arusha Mjini - CCM**



Godbless Lema
**Arusha Mjini - CHADEMA**



Saashisha Mafuwe
**Himo - CCM**

## Arusha Mjini na Hai majimbo pasua kichwa kwa wapigakura

UKURASA 3



Freeman Mbowe
**Himo - CHADEMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akifunua kipazia kuzindua Jengo la Maduka ya Kisasa la Sheikh Thabit Kombo Kisonge Michezani jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa. **PICHA: IKULU**

# Mvutano Msajili, upinzani wapamba moto

**Na Mary Geofrey**

MVUTANO kati ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na vyama viwili vya siasa; CHADEMA na ACT-Wazalendo, Msajili akikemea kuungana kwa vyama kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu huku vyama hivyo vikisisitiza kutorudi nyuma katika azma yake ya kushirikiana.

Kwa takriban wiki moja sasa, kumekuwa na mvutano baina ya pande hizo mbili, Ofisi ya Msajili ikidai kuna uvunjaji wa sheria vyama kutaka kuungana, huku vyenyewe vikidai havijavunja sheria husika.

Huku Msajili asisitiza ofisi yake kutofumbia macho suala hilo, Chama cha ACT-Wazalendo jana kilisambaza kwa vyombo vya habari barua yenye kumbukumbu namba HA, 322/362/21/90 kiliyoiandika Septemba 22 mwaka huu kuijibu Ofisi ya Msajili iliyokitaka kiwasilishe maelezo kuhusu mgombea wake wa urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, kudaiwa kumwombea kura mgombea wa urais wa Tanzania, Tundu Lissu.

Barua hiyo iliyoandikwa na Ofisi ya Katibu Mkuu wa chama hicho, ilirejea barua waliyoandikiwa na Ofisi ya Msajili ikiwakumbuha uwapo kwa Kifungu cha 11A cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinachoweka utaratibu wa vyama kushirikiana na kukiuka ni kuvunja sheria.

"Tunapenda kueleza kuwa mgombea wetu wa urais wa Zanzibar, Seif Sharif Hamad, hajakiuka kifungu cha 11A cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kinachoweka utaratibu wa vyama kuungana au vinavyokusudia kuungana kabla au baada ya uchaguzi," inasomeka sehemu ya barua hiyo.

Chama hicho kupitia barua yake hiyo, kinadai kuwa Maalim Seif hakumwombea kura Lissu kama inavyodaiwa na Ofisi ya Msajili na kwamba kipande cha video iliyotumiwa hakina maneno ya kumwombea kura mgombea huyo.

"Alichokisema Maalim Seif ni imani yake kwa Lissu atakuwa Rais wa Tanzania jambo ambalo lipo wazi sana kutokana na mwelekeo wake wa kuungwa mkono na Watanzania walio wengi.

"Hili siyo kosa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Kwa maelezo hayo, ni matumaini yetu kuwa sasa utakuwa umefahamu maana ya tafsiri sahihi na tofauti ya vyama kuungana chini ya kifungu cha 11A cha Sheria ya Vyama vya Siasa na mgombea mmoja kuonyesha imani yake kwa mgombea mwingine katika uchaguzi huu," ilielezwa zaidi katika barua hiyo ya ACT-Wazalendo.

Wakati ACT-Wazalendo wakiyasema hayo, CHADEMA kupitia kwa Katibu Mkuu wake, John Manyika, iliiambia Nipashe jana kuwa kinachoendelea kinawapa hisia za Ofisi ya Msajili kutumika kuviumiza baadhi ya vyama vya upinzani kwa kuwa hawajawahi kutangaza kuunda muungano wa vyama.

Alidai hawajakiuka kifungu cha 11A cha Sheria ya Vyama vya Siasa na kwamba kutaka mgombea wa chama kingine achaguliwe siyo kosa kwa mujibu wa sheria.

"Hatutarudi nyuma, suala hili tutatoa taarifa zaidi kupitia mkutano wetu na waandishi wa habari kesho (leo)," alisema Mnyika.

**KAULI YA MSAJILI**

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akihojiwa na BBC juzi, alisema hawataruhusu wagombea au vyama vilivyosimamisha wagombea, kuungana kwa sababu kufanya hivyo ni kuvunja sheria na kuwachanganya wananchi.

Alisema kabla ya kuanza kwa mchakato wa kampeni za uchaguzi, walikaa na viongozi wote wa vyama vya siasa na kuwaeleza mambo ya kuzingatiwa, lakini bado kuna vyama vinakiuka sheria na taratibu.

Alisema tayari wameshaviandikia barua CHADEMA na ACT-Wazalendo kuhusu ukiukwaji wa sheria unaodaiwa kufanywa na vyama hivyo.

"Mgombea wa CHADEMA, alimnadi wa ACT-Wazalendo, tumeshawaandikia barua na vilevile wa ACT-Wazalendo alimnadi mgombea wa CHADEMA, tumeshamwandikia barua. Tunaendelea kuchukua hatua. Kwanza, tulikutana nao kuwaasa kuzingatia sheria na hatutaruhusu kuvunja sheria," alisema Nyahoza.

Mwanasheria Frugence Massawe akizungumzia suala hilo, alisema lina mkanganyiko kwa sababu Sheria Sheria Na. 1 ya Uchaguzi ya Mwaka 2019 kifungu cha 11A kinaeleza namna ya kuungana kuanzia hatua ya mchakato hadi kupeleka maombi yao kwa Msajili.

Alisema sheria hiyo iliyofanyiwa marekebisho mwaka jana, haijakataza ushirikiano wa vyama vya siasa usio rasmi.

Alitolea mfano ushirikiano usio rasmi ni mkutano mkuu wa ACT-Wazalendo kumwalika Tundu Lissu ambaye katika mkutano huo pia alipata fursa ya kuhutubia.

Alikumbusha kuwa hata mkutano mkuu wa CCM uliofanyika Dodoma mwaka huu ulialika vyama vingine vya siasa na kupewa fursa ya kusalimu zao.

"Hiyo ni mifano ya ushirikiano usio rasmi ambao sheria haijakataza ushirikiano kama huo," alisema Massawe.

Mwanasheria huyo pia alirejea uamuzi wa Chama cha TLP wa kutangaza kumuunga mkono mgombea urais wa CCM, John Magufuli na kuweka bayana kuwa ndiye mgombea wa TLP, nao ni ushirikiano usio rasmi.

Alisema demokrasia nchini bado haijakua kama mataifa mengine ambayo vyama vinaweza kutangaza msimamo wake kuhusu mgombea anayeonekana kufaa na suala hilo siyo kosa kisheria.

# CCM yataja mikakati 6 kupambana na majanga

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimejinasibu kuja na mikakati sita ya kukabiliana na magonjwa hatari ya mlipuko nchini kwa miaka ijayo, ikitoa mfano wa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona ulivyoitesa dunia.

Kimesema kitahakikisha nchi inakuwa na utayari wakati wote wa kuzuia, kudhibiti na kukabiliana na majanga ya magonjwa hayo, kwa kushirikiana na wadau wengine.

Kwa mujibu wa ilani ya chama hicho ukurasa wa 139, CCM kimeeleza kuwa, kutokea kwa ugonjwa wa corona duniani na kuiathiri Tanzania, kumetoa funzo ya kuwa na umuhimu wa kujipanga kikamilifu katika kukabiliana na majanga ya aina hiyo, yanapojitokeza.

Kimeeleza kuwa kitahakikisha kinaihamasisha serikali kuweka, kuimarisha mifumo na miundombinu ya kutambua, kudhibiti na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko pamoja na yale yanayoenea kwa kasi.

Pili, kitahakikisha serikali inaimarisha mpango wa taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, ajali na majanga kwa kuboresha huduma za dharura na uokoaji ikiwamo miundombinu na vitendea kazi.

Tatu, kuaimarishwa na kujengwa uwezo wa kufanya utafiti kuhusu magonjwa ya mlipuko katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa magonjwa ya binadamu (NIMR), vyuo vikuu na taasisi nyingine za utafiti nchini.

"Magonjwa ya mlipuko na yanayosambaa kwa kasi ni hatari kwa maisha ya wananchi na ulinzi na usalama wa Taifa, CCM itahakikisha nchi inakuwa na utayari wakati wote wa kuzuia, kudhibiti na kukabiliana na majanga haya kwa kushirikiana na wadau wengine," ilieleza Ilani hiyo.

Mkakati wanne ni kuanzisha kituo kikubwa cha utafiti na uchunguzi wa mimea dawa na kuanzisha kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa, zitokanazo na mimea ya asili.

Kimeeleza kuwa mkakati wa tano ni kuimarisha uwezo wa wataalam waliopo nchini katika kuzuia na kutibu magonjwa ya mlipuko kwa kupatiwa vifaa na mafunzo ndani na nje ya nchi.

Pia, kimesema kitahakikisha kunajengwa na kuimarisha maabara za uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko, vituo vya kisasa vya kuwatenga wahisiwa wa magonjwa hayo na kutoa tiba kwa wagonjwa.

Wakati huohuo, imesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitaendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya afya kwa kuwa inagusa maisha ya Watanzania na ustawi wa taifa.

Lengo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya na siha bora, ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za ujenzi wa taifa na kuboresha maisha yao.

Kadhalika, kitaisimamia serikali kuhakikisha inaimarisha huduma za afya ya mama na mtoto na kuzitoa bila ya malipo, ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Pia, kitahamasisha serikali kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi kulingana na mahitaji katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini.

Vile vile, kuhakikisha serikali inaweka mazingira kwa wawekezaji, sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi kwa kutumia malighafi zinazopatikana ndani ya nchi, ili kupunguza mzigo kwa serikali wa kuagiza mahitaji hayo kutoka nje ya nchi.

## HABARI KITAIFA

# Arusha Mjini na Hai majimbo pasua kichwa kwa wapigakura

**Na Godfrey Mushi,** HAI

NI majimbo pasua kichwa. Ndivyo ambavyo inaonekana ndani ya majimbo ya Arusha Mjini mkoani Arusha na Hai, Kilimanjaro kutokana na sababu kuu mbili.

Sababu ya kwanza ni ya kisiasa ambayo imejengeka ndani ya majimbo hayo, hasa kutokana na upinzani mkali kati ya chama tawala- Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Sababu ya pili ni wagombea kutokana na mvuto, ukomavu wa kisiasa na umaarufu wao katika medani hiyo.

Upinzani huo wa kisiasa ulianza tangu kuasisiwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na vyama hivyo viwili kwa miaka mingi vimekuwa vikichuana kila ifikapo wakati wa uchaguzi, hivyo kuwa vigumu kubashiri nani anaweza kuibuka mshindi.

Katika Jimbo la Hai, ni vigumu kuzielezea siasa za eneo hilo bila kutaja jina la Freeman Mbowe. Huyu ni mwanasiasa aliyekomaa na mpinzani asiyekata tamaa, aliyeongoza CHADEMA ambacho ni chama kikuu cha upinzani.

Huyu ni mwanasiasa ambaye amekuwa mwiba na kisiki dhidi ya CCM katika kulitwaa jimbo hilo mara nyingi ikiwamo katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Ni mtu wa aina yake, anayejua kucheza na propaganda na mjanja wa kuvuruga mipango yake ya ufanyaji wa kampeni ili kumdhibiti mpinzani wake kugawa kura na kumshinda kirahisi.

Wakati anazindua kampeni zake katika Kata ya Narumu Wilaya ya Hai, Mbowe aliahidi kama wakazi wa jimbo hilo watamchagua kwa kipindi cha tatu, atasimamia vipaumbele vitatu pekee katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alisema yuko tayari kuzipigania ndani na nje ya Bunge na anawapa uhakika wanaompinga kwamba hayo mambo yanawezekana. Katika mkutano huo, alisema amesikia mara nyingi kilio cha watu wa Narumu cha kukosekana kwa barabara ya uhakika kufika katika maeneo yenye huduma muhimu za kijamii.

"Mkinichagua tena kuwa Mbunge wa Hai, nawahakikishia serikali inayoongozwa na CHADEMA itajenga barabara hii. Katika barabara kipaumbele changu kwenye Jimbo la Hai ni barabara ya Narumu/Mnadani/Weruweru.

"Barabara hiyo inapita Narumu inakwenda Lyamungo inashuka Makoa, inapita Nkuu inaishia Makoa, inaunganisha lami ya pale, inakwenda kuunganisha babarara inayokwenda Isareni, Mula inashuka kwa Sadala."

Aidha, Mbowe alisema kipaumbele cha pili ni barabara inayotoka Bomang'ombe Mjini inashuka mpaka Rundugai, inakamata ukanda wa tambarare wenye kilimo kikubwa, inakwenda mpaka Kikavu Chini.

Kipaumbele cha tatu ni lami inayounganisha barabara ya Masama Magharibi na Masama Mashariki na kushuka mpaka Kware.

**MAFUWE KISIKI CHA MBOWE**

Mgombea ubunge wa Jimbo la Hai, kwa tiketi ya CCM, anatajwa kuwa kisiki kwa Mbowe kupata tena ubunge. Ana ushawishi, anaungwa mkono na matajiri na wengi wanamchukulia kama kijana anayeweza kuiteka Hai na kufanya mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

Mara kadhaa katika mikutano yake ya kampeni amesikika akiahidi zaidi kuhusu mageuzi ya kilimo na viwanda, wakati Tanzania ikiwa imeingia katika orodha ya nchi za uchumi wa kipato cha kati.



Mrisho Gambo

Hisia za baadhi ya wapiga kura wa Hai wanaomzungumzia Mafuwe, mwanafunzi wa Shahada ya Udaktari wa Falsafa (PhD) katika Chuo Kikuu cha Dodoma, wanamwona ndiye nuru mpya ya maendeleo kwa Jimbo la Hai.

Mmoja wa wananchi hao, Kayfa Athuman, anasema bila Mafuwe maji yataendelea kuwa kero kuu, barabara hazitajengwa kwa kiwango kile kinachohitajika.

Lakini Zainab Mwasha, mkazi wa Gezaulole, anasema ingawa wanataka CCM ishinde ubunge katika jimbo hilo, changamoto kubwa anayoiona na mgombea huyo kutojulikana sana.

**ARUSHA MJINI**

Katika Jimbo la Arusha Mjini nako ni patashika nguo kuchanika. Hiyo ni kutokana na kuwapo kwa wagombea wanaochuana vikali nao si wengine bali ni Godlbess Lema wa CHADEMA na Mrisho Gambo wa CCM.

Licha ya kuwa na wagombea wenye umaarufu, mtifuano mwingine baina ya vyama hivyo ni kuwapo kwa wafuasi wenye nguvu kila upande. Wagombea hao pia wamekuwa na sera nyingi ambazo kwa mtazamo au fikra ya kawaida kuna sera zinazotekelezeka na zile zisizotekelezeka.

Hadi sasa, Lema, ameshafanya mikutano 13 ya kampeni katika kata za Jiji la Arusha na kunadi sera zake huku hoja yake kubwa ikiwa kurejesha hadhi ya sekta ya utalii iliyoathiriwa na corona.

Katika kujinadi huko, Lema amekuwa akisisitiza kuwa endepo atachaguliwa kwa mara ya tatu kuwa mbunge wa jimbo hilo, atahakikisha anasimamia sekta hiyo kupiga hatua ili iwanufaishe wananchi wa mkoa wa Arusha.

Amekuwa akikaririwa kuwa kutokana na corona, sekta ya utalii imeathiriwa na kwamba kwa kuwa utalii ni kazi tegemeo kwa wananchi wa Arusha, akiwa mbunge atapambana kuirudisha kama ilivyokuwa mwanzo huku akiahidi kupeleka muswada bungeni wa kufutwa kwa kodi ambazo zimekuwa kikwazo kwa maendeleo ya sekta hiyo.

Turufu yake nyingine imekuwa kujenga jengo la wamachinga kufanyia biashara (Machinga Complex) ili kutengeneza ajira rasmi na kuondoa adha kwa wafanyabiashara hao kufanya shughuli zao kandokando ya barabara na kuzunguka mitaani.

Pia amekuwa akijinadi kuwa kwa kipindi cha miaka 10 ya ubunge wake, amesimamia utekelezaji wa miradi ya afya, maji, elimu na ujenzi wa barabara ndani ya Jiji la Arusha.

Licha ya kuonekana bado ana nguvu, Lema anakabiliwa na kigingi kizito kupenye tena kuwa mbunge wa jimbo hilo kutokana na CCM kumweka Mrisho Gambo, ambaye kabla ya hapo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Kwa mantiki hiyo, Gambo kwa maneno mengine, anaonekana ni 'mtoto wa mjini' katika Jiji la Arusha na atamtikisa Lema ipasavyo katika kinyang'anyiro hicho.

Katika mikutano yake, Gambo amekuwa akiahidi kuwa akichaguliwa kuwa mbunge, atatatua tatizo la madaraja katika kata za Osunyai na Sombeni kupunguza adha ya mafuriko nyakati za mvua.

Pia amekuwa akijinasibu kwamba atahakikisha huduma za maji, umeme, barabara na afya zinawafikia wananchi wote wa Jiji la Arusha na kwamba atahakikisha vikundi vyenye sifa vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, vinapata mkopo wa asilimia 10 unaotolewa na Halmashauri ya Jiji la Arusha kila mwaka wa fedha.

Aidha, anasema kwa kuwa Arusha ni kitovu cha utalii, ataendeleza amani iliyopo ili watalii waendelee kuja nchini kwa wingi.

# Ufafanuzi

**KATIKA toleo letu la jana, tulichapisha kwenye ukurasa huu habari yenye kichwa kilichosomeka 'Fatma Karume akwaa kigingi kingine, TLS yamtia hatiani', ikieleza kwamba Kamati ya Maadili ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), imeondoa jina la Fatma Karume katika orodha ya mawakili.**

**Baada ya ufuatiliaji wa kina, tumebaini hatua hiyo imechukuliwa na Kamati ya Maadili ya Mawakili nchini iliyomkuta na hatia ya kukiuka maadili ya uwakili na siyo Kamati ya TLS.**

**Kamati iliyochukua hatua hiyo iliundwa kwa mujibu wa sheria za nchi na wajumbe wake ni pamoja na Jaji kutoka Mahakama Kuu ambaye anakuwa mwenyekiti wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au naibu wake au Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na wakili aliyethibitishwa na TLS.**

**Tunaiomba radhi TLS na wasomaji wetu kwa usumbufu uliojitokeza.**

**Mhariri**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TANGAZO KWA UMMA**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inawaalika mafundi umeme wote wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwenye semina ya siku tatu (3) itakayoanza saa tatu (3) asubuhi, tarehe **30/09/2020** hadi tarehe **02/10/2020.** Semina itafanyikia ukumbi wa Baraza la **Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)** uliopo Mikocheni eneo la Viwanda.

Baadhi ya mambo yatakayofundishwa ni pamoja na namna ya kupima vitu muhimu kama vile earth resistance, insulation resistance na earth loop impedance katika mfumo wa umeme.

**Jinsi ya kufika ukumbini:** *kutokea Kituo cha basi ITV, fuata barabara inayokwenda Chuo cha Kodi Mikocheni, elekea upande wa kulia.*

Kwa mafundi watakaopenda kuhudhuria wathibitishe ushiriki wao kabla ya tarehe 29/09/2020 kwa kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi **(SMS) 0754 26 59 36 au piga +255222123850/3/4/6.**

**MAFUNZO HAYA NI BURE KABISA**

**Limetolewa na**

**MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

215915402

# Mwanafunzi matatani tuhuma kumkata mapanga mwalimu

**Na Asha Shabani,** MUSOMA

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Kiaga wilayani Butiama, mkoani Mara, anashikiliwa na Jeshi la polisi kwa tuhuma za kumkata mapanga na kumsababishia majeraha mwalimu.

Inadaiwa kuwa chanzo ni utoro shuleni na kuamriwa kuita wazazi shuleni.

Kamanda wa Polisi mkoani Mara, Daniel Shillah, alisema tukio hilo limetokea shuleni majira ya asubuhi wakati mwalimu akiwa anakagua wanafunzi watoro ndipo mwanafunzi huyo alimkata panga mwalimu wake wakiwa darasani.

Alisema mwanafunzi huyo amekuwa na tabia ya kutodhuria shuleni mara kwa mara, jambo ambalo liliwalazimu walimu kumuandikia barua ya kuita wazazi ili wajue sababu za kutohudhuria mara kwa mara.

Shillah aliongeza kuwa wakati mwalimu huyo akikagua wanafunzi watoro darasani, alimuuliza mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) sababu ya kutokuja na wazazi wake, ndipo alipochomoa panga alilokuwa amelificha ndani ya nguo zake za shule na kuanza kumkatakata mwalimu sehemu ya bega la kulia na kiganja cha mkono wa kushoto.

Kamanda huyo alisema walifanikiwa kumtia mbaroni mwanafunzi huyo, na kuwa yupo mahabusu akisubiri uchunguzi kukamilika ili afikishwe mkortini.

**MWALIMU ASIMULIA**

Mwalimu huyo, Majogoro John, alisema wakati anaita majina ya wanafunzi watoro darasani hapo alimuona mwanafunzi huyo na kumuuliza kwanini hakuchukua barua ya kupeleka kwa wazazi wake, lakini mwanafunzi huyo hakumjibu kitu, badala yake akasubiria wakati anatoka darasani ndipo akachomoa panga alilokuwa na kuanza kumkatakata.

Alisema alipoona mwanafunzi huyo anamsogelea akamgeukia na kukatwa panga la begani upande wa kulia na kwamba wakati anajiandaa kukabiliana nae, akamkata tena kwenye kiganja cha mkono wa kushoto ukawa unaning'inia kisha mtuhumiwa alikimbia kutoka eneo la tukio.

**MAELEZO YA HOSPITALI**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, Dk. Joachim Iyembe, amesema walimpokea majeruhi huyo na kumfanyia uchunguzi wa awali na kubaini kuwa sehemu iliyojeruhiwa zaidi ni mkono wa kushoto ambapo mifupa miwili imekatika na kusababisha mishipa ya fahamu kutokufanya kazi .

Iyembe alisema kuwa kutokana na kuhitaji huduma za matibabu zaidi hospitali ya mkoa imeamua kumpa rufani ya kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Nayo ofisi ya mkuu wa mkoa imetoa tiketi ya ndege kwa ajili ya mwalimu huyo kupelekwa Muhimbili jijini Dar es Salaam haraka, huku hospitali ya mkoa ikitoa gari kwa ajili ya kumfikisha mgonjwa huyo jijini Mwanza kwa ajili ya kupanda ndege.



Mwalimu Majogoro John, anayedaiwa kujeruhiwa kwa panga na mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Kiaga, wilayani Butiana, akiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara kwa matibabu. **PICHA: ASHA SHABANI**

## Utaratibu tamko mali za viongozi kisiasa kutolewa

**Na Frank Maxmillian,** TUDARCO

SEKRETARIETI ya maadili ya viongozi wa umma imesema, viongozi wa siasa wanaoshiriki uchaguzi mkuu, watapewa utaratibu wa ujazaji wa tamko la rasilimali na madeni kwa mujibu wa sheria ya viongozi wa umma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna wa Maadili Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa vyombo vya habari, viongozi wengine wanatakiwa kutekeleza wajibu huo wa kisheria.

"Viongozi watatakiwa kujaza upya mali zao zote, ili kujaza na kuwasilisha tamko, viongozi watatumiwa taarifa za siri kwa njia ya ujumbe mfupi kwenye simu zao za mkononi, maadili au barua pepe."

Alisema mfumo wa ujazaji wa tamko la rasilimali na madeni kwa njia ya mtandao "online declaration system ods" umeanza kutumika tangu Aprili, mwaka huu, uliojengwa chini ya ufadhili wa mkakati wa kujenga mpango endelevu wa mapambano dhidi ya rushwa.

"Ujazaji tamko ni matakwa ya kisheria yaliyotajwa na sheria ya maadili ya viongozi wa umma, linamtaka kiongozi wa umma kila mwisho wa mwaka kumpelekea kamishna wa maadili, tamko la maandishi katika hati rasmi, linaloonyesha mali na rasilimali zake, mwenza au wenza na watoto walio chini ya umri wa miaka 18, ambao hawajaoa au kuolewa."

# Mfanyabiashara matatani tuhuma za kumweka mwanafunzi kinyumba

**Na Elisante John,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa nchini (TAKUKURU), Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, inamshikilia mfanyabiashara na ofisa masoko wa kiwanda kimoja kinachotengeneza sufuria mwenye asili ya kiasia, Ashrafal Mohamed (51), kwa tuhuma ya kumbaka na kumweka kinyumba msichana wa kidato cha pili.

Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Ikungi, Erick Nyoni, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa, mfanyabiashara huyo mkazi wa jijini Dar es Salaam, anadaiwa kutoweka na msichana huyo na kwenda kuishi naye jijini humo tangu Juni 14, mwaka huu, wakati mwanafunzi akiwa likizo ya lazima iliyotolewa na serikali, kutokana na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Kamanda Nyoni alisema, walifanikiwa kumtia mbaroni mtuhumiwa akiwa kwenye moja ya nyumba za kulala wageni iliyopo kijiji cha Puma, ambako walifikia wakiwa na mwanafunzi huyo, akiwa njiani kwenda nyumbani kwa msichana, kwa ajili ya kwenda kutekeleza ahadi yake ya kumjengea nyumba inayogharimu mabati 32.

"Baada ya kupata tukio hili tangu mwezi wa sita tumekuwa tukimtafuta, tunashukuru sana ushirikiano wa ndugu, jamaa na wananchi wa Kijiji cha Kipumbuiko, anakoishi mwanafunzi huyo wa umri wa miaka 16, wametupa ushirikiano mkubwa hadi juzi tulipomkamata akiwa amerudi kwa ajili ya kuja kujenga nyumba aliyomwahidi mwanafunzi... mwanafunzi tulimkuta kwenye nyumba moja ya wageni iliyopo kijiji cha Puma, ambako walifikia wote wawili," alifafanua Nyoni.

Wakati TAKUKURU Wilaya ya Ikungi, ikitahadharisha jamii kuacha mazoea ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, baadhi ya walimu wa shule anakosoma mwanafunzi huyo akiwamo mwalimu wa kidato cha pili 'B' Maria Ntandu na Makamu mkuu wa shule Mario Msengasi, walisema kuwa watampokea, ili aweze kuendelea na masomo baada ya kuonana naye na kuonyesha nia ya kuendelea na elimu, huku wakieleza namna alivyotoweka.

Walisema kuwa, awali mwanafunzi alikuwa akihudhuria vyema masomo kabla ya shule kufungwa kutokana na ugonjwa wa Covid-19, lakini zilipofunguliwa, hakurudi shuleni, huku wakipokea taarifa kwamba alitoweka baada ya kurubuniwa na mtuhumiwa aliyefanikiwa kufika kijijini hapo, kuhudhuria moja ya sherehe za familia, wakati huo akiwa na uhusiano wa kimapenzi na mama mdogo wa mwanafunzi.

Kutokana na tukio hilo, baadhi ya wazazi wa kijiji cha Kipumbuiko akiwamo Athuman Mkoha, anakoishi mwanafunzi huyo na viongozi wa kata ya Siuyu, Yahaya Njiku, ambaye ni Ofisa mtendaji wa kata, wilayani Ikungi, wamelaani tukio hilo, huku wakiiomba serikali kuchukua hatua kali kwa wanaume wenye tamaa dhidi ya wasichana wa shule, hali inayosababisha wasifikie ndoto zao za kuwa na maisha bora siku za usoni.

Kwa mujibu wa Kamanda Nyoni, mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote, kutokana na upelelezi wa shauri lake kukamilika.

# ACT yatamba 'kunyakua' majimbo Tunduru

**Stevie Chindiye**, TUNDURU

CHAMA cha ACT-Wazalendo wilayani hapa kimetamba kupata ushindi wa kishindo kwenye majimbo ya Tunduru Kaskazini na Kusini katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa chama hicho taifa na mgombea ubunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, Ado Shaibu, alisema hayo wakati akiongea na wananchi walioji-tokeza kwenye mapokezi ya wagombea wa chama hicho yaliyofanyika Kijiji cha Sisikwasisi hadi makao makuu ya chama hicho Tunduru Mjini.

Akifafanua taarifa hiyo, Shaibu alisema wingi wa wananchi waliojitokeza katika mapokezi hayo kunaonyesha kukubalika kwa wagombea walioteuliwa kupeperusha bendera ya chama hicho katika majimbo ya Tunduru Kusini linalowaniwa na Mtutura Abdalah Mtutura na Ado Shaibu wa Tunduru Kaskazini.

Mgombea wa chama hicho katika Jimbo la Tunduru Kusini, Mtutura, alisema mapingamizi ya CCM yaliyowekwa dhidi yao yalilenga kuwasaidia wagombea wa chama hicho kupita kwa mtelezo hivyo ushindi kwenye majimbo yote kwa ACT-Wazalendo upo wazi.

Alisema baada ya kuwekewa mapingamizi hayo, waliamua kwenda jijini Dar es Salaam na kuandika rufani ambazo zimewashawishi viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kurudisha majina yao ili waingie kwenye kinyang'anyiro hicho hatua inayo wahakikishia kuibuka na ushindi kupitia sanduku la uchaguzi Oktoba 28.

Awali, Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Wilaya ya Tunduru, Mohammed Mawila, aliwaeleza wananchi hao kuwa watarajie kampeni za ustaarabu katika kipindi chote cha kampeni na kwamba siku ya uzinduzi watakuwapo viongozi wa kitaifa wa chama hicho na watashiriki kubadilishana hadi mwisho wa kampeni hizo kwa ajili ya kuwanadi wagombea wa nafasi za urais, ubunge na udiwani.



Mjumbe wa Kamati Kuu na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasalimia wananchi wa Kata ya Misungwi, wilayani Misungwi, mkoani Mwanza, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu jana. **PICHA: OWM**

# Majaliwa awapa somo wapigakura

**Na Neema Emmanuel,**

MISUNGWI

WANANCHI wa Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza wametakiwa kufanya uamuzi sahihi na kumpigia kura kiongozi, atakayewaletea maendeleo bila kujali tofauti za vyama.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, alitoa somo hilo wakati akizungumza na wananchi wa Jimbo la Misungwi katika kampeni za uchaguzi.

Majaliwa alikuwa Misungwi kumwombea kura mgombea wa urais wa CCM, Dk. John Magufuli na wagombea ubunge na udiwani wa chama hicho.

Alisema, maendeleo hayana chama hivyo ni vyema wakamchagua kiongozi atakayeweza kuchapa kazi na kuleta maendeleo kwa Watanzania wote wakiwamo wanyonge.

Alisema wametekeleza miradi mbalimbali ikiwamo, maji na sasa wanateknolojia mpya ya kutoa maji ziwani, kwenda kwa wananchi.

Aliwataka wananchi hao kuwapeleka shule watoto kwa kuwa sekta hiyo imeboreshwa kwa kiwango kikubwa, pia mchakato wa kujenga mabweni kwenye shule za sekondari unaendelea.

Aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Charles Kitwanga, akizungumza na wananchi hao alisema serikali imefanya mambo mengi ikiwamo ujenzi wa hospitali mpya.

"Fedha za mradi huo wa maji Usagara, zimetoka mdogo wangu (Mnyeti) zisimamie hizo fedha zisije zikaenda kusikojulikana, usimamie vyema usije ukafanya mambo yetu yale mengine, kwa sababu CCM inasimamia maadili," alisema Kitwanga.

Naye mgombea wa ubunge wa Jimbo la Misungwi kupitia CCM, Alexander Mnyeti, alisema anachosubiri sasa ni kuwafanyia kazi wananchi hao.


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **Harbor Microfinance Company Limited** sisi **J & J Recoveries** tunatoa taarifa kwa mdaiwa kulipa deni unalodaiwa ndani ya siku 14 ya tangazo hili, baada ya hapo tutapiga mnada dhamana (nyumba) iliyo orodheshwa hapo chini.

| JINA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| MWAMVITA HUSSEIN MPAHI | NYUMBA | MAJOWE, KICHANGANI WILAYA YA ILALA | KUANZIA 9/10/2020. |


# Serikali yaboresha miundombinu usafiri

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa amesema serikali imeimarisha miundombinu ya usafiri nchini ili kuwawezesha wananchi kuchagua aina ya usafiri wanaotaka.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wakazi wa Misungwi kwenye mkutano uliofanyika kwenye uwanja wa Amani, Misungwi mkoani Mwanza.

"Tunataka tuhakikishe Watanzania wanatumia njia zote za usafiri kulingana na matakwa yake ndiyo maana tunatengeneza barabara, tumenunua ndege, tunajenga reli pamoja na kuendelea kuboresha usafiri wa majini," alisema.

"Tunajenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Dodoma, baadaye itatengenezwa ifike hadi Tabora na Mwanza. Ukitaka kupanda ndege una uhuru, ukitaka treni nenda, ukitaka basi, barabara nzuri zipo na ukienda majini nako pia tumeboresha usafiri," aliongeza.

Majaliwa yuko mkoani Mwanza kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Pombe Magufuli.

Aliwasisitiza wakazi hao wasiache kupiga kura siku hiyo. Mbunge wa jimbo la Misungwi, Alexander Mnyeti na wagombea wote 27 wa udiwani wa jimbo hilo wamepita bila kupingwa.

"Tunataka tuwe na kiongozi ambaye anaweza kuratibu maendeleo ya Watanzania. kiongozi ambaye anaweza kurudi chini na kujua kuna changamoto gani. Tunataka kiongozi ambaye ana uwezo wa kusimamia rasilimali zetu na huyo si mwingine bali ni Dk. John Pombe Magufuli," alisema.

Kuhusu mifugo, Majaliwa alisema: "Rais wetu amefanya maboresho makubwa sana katika sekta ya mifugo. Rais anataka kuona wafugaji na wavuvi wananufaika na shughuli zao, yale mapori makubwa tunachukua ili wafugaji wapate sehemu za malisho pia tunajenga mabwawa hukohuko. Tunajenga maabara kwa ajili ya kutibu mifugo yetu. Kwenye uvuvi tunaimarisha sekta hiyo, ili kuhakikisha tunaendelea kuinua sekta hiyo, tumepunguza kodi pamoja na kuondoa tozo mbalimbali."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi uanzishe vipaumbele vya 50/50

**SUALA** la wanawake kushiriki kwenye uchaguzi mkuu limekuwa likijadiliwa na jamii kutokana na ukweli kwamba hawajapewa nafasi kikamilifu kwenye uchaguzi huu hasa majimboni.

Zimebakia siku chache kabla ya uchaguzi, hivyo habari ya majimbo sasa zinafikia mwisho kwa sababu hakuna tena kutiania wala kuchukua fomu, mchakato huo umeshafungwa na cha msingi ni kinamama kujipanga na kuamini kuwa wanaweza na wana nafasi.

Wakati wa kujipanga ni jambo la msingi kufahamu kuwa wanawake hawawezi kufanikiwa peke yao ni lazima kuwa na umoja. Hivyo wanahitaji kuungwa mkono na wenza wao (wanaume), wana ndugu na familia, mifumo, sheria na taratibu ambazo zinaelekeza ushiriki kikamilifu wa wanawake katika masuala ya siasa.

Hivyo suala la kuwa na ushiriki mkubwa wa wanawake, lisiishie kwenye uchaguzi pekee bali kikubwa kuanzia sasa ni Tanzania kuwa na 'gender equality attitude', mtizamo wa kuwa na usawa wa kijinsia ambao kila mmoja ataamini na kuamini kuwa hakuna kitu mwanamke asichokiweza.

Mathalani, Tanzania imewahi kuwa na mawaziri wa fedha wanawake kwanza Amina Salim Ali, Zakia Meghiji na Saada Salum Mkuya, ni wakati ambao taifa lilivunja mwiko kwa wakuu wa nchi kuteua wanamama kuongoza wizara nyeti.

Inafahamika kuwa tangu uhuru wanaume wamekuwa wakiongoza wizara hiyo nyeti na muhimu ya nchi na iliyoonekana kama eneo maalumu kwa wanaume wakiwamo maprofesa na madokta na iliyochukuliwa kuwa hakuna mwingine anayeiweza.

Wanawake wameiongoza na wamefaulu na sasa si wakati wa kulalamikia uchaguzi na kampeni bali waanze kujiweka sawa na kujiamini, huku wakiondokana na hisia kuwa hawataweza. Ni muda wa kuanza kujipa moyo na kujiamini kuwa wanaweza na kuachana na hofu za kiupungufu wa kutokujiamini. kwa kujiambia nipo tayari kwanini nisiweze? Wanawake waanze kujiuliza kwani kigumu ni kipi? Kinamama wengi wanafanyakazi kazi zenye changamoto tena katika mazingira magumu kuna wakati wanakabiliana na njaa, mafuriko, magonjwa na wanatimiza jukumu hilo kwa kusaidia jamii zao, familia na wananchi.

Kwa hiyo kuna haja ya kujiamini na kuwa na imani kuwa inawezekana si katika uchaguzi mkuu pekee bali katika majukumu mengine yote. Kuna haja kwa wanawake kujituma na kufanyakazi zaidi, kuwa na bidii kwa kuhakikisha kuwa taifa linapata manufaa kutoka kwa wanawake kwa kuondoa mifumo, sheria, taratibu na vikwazo vinavyowaelemea. Ili kuwapa kinamama nafasi zaidi taifa linahitaji kuwa na mfumo unaosimamiwa na serikali utakaowapa nafasi wanawake na kufikia Tanzania inayowapa wanawake na wanaume fursa sawa.

Nguzo kuu iwe uongozi na utawala bora, kusaidia kuimarisha uongozi makini, kuendeleza demokarasia, uongozi unaozingatia usawa wa kijinsia. Taifa liwe na maono kwamba kuna haja ya kubadilisha mitizamo na kuachana na mambo ya nyuma yanayotishia ustawi wanawake, utawala bora na demokrasia.


Ni muda wa kukubali kujenga mifumo bora ya kidemokrasia na kuhakikisha uwepo wa uongozi unaoheshimu haki za wanawake na wanaume, watoto, wahitaji, wazee na makundi yote.

Kwa wananchi kila mmoja aone kuwa kuna tofauti, hakuna ubaguzi, unyanyasaji, mauaji ya wanawake hasa vikongwe, mimba na ndoa za utotoni na manyanyaso ya aina yoyote.

Maisha baada ya uchaguzi yahakikishe kuwa dukuduku za watu kutaka ushiriki zaidi wa wanawake zinasikilizwa na kufanyiwa kazi kikamilifu.

Lakini pia, tunaona kuwa ni vyema kama inawezekana kuwa na mijadala ya kitaifa au wa vyombo mbalimbali kuwaleta kwa pamoja wanasiasa, wanazuoni, viongozi wa dini na asasi za kiraia na umma kujipanga kikamilifu ili kuwapa wanawake nafasi zaidi za kushiriki kwenye siasa na uongozi kwenye ngazi za kutoa maamuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kivutio safi, mkakati wa shule kuinua walio chini wang'are

**MIKAKATI** ya kuwakomboa kiuwezo wanafunzi walio chini kimasomo, inatakiwa kuandaliwa katika namna ya kuwawezesha wanafunzi kusoma na kuelewa .

Wapo wanafunzi ambao wanakuwa na uwezo wa chini kimasomo, lakini wanaposimamiwa wanapanda kwa uwezo wa kubadilika na hata kufanya vizuri kwa wanayotakiwa kitaaluma.

Wapo baadhi ya wanafunzi ambapo wanakabiliwa na matatizo mbalimbali kitaaluma. Lakini wanapokuwa shuleni, daima huwa kunakuwapo mikakati ya haraka kuwatafutia majibu, hata kilichowakuta kubaki historia.

Hapo huwa ni wajibu wa walimu kuzifuatilia matatizo hayo kwa ukaribu, kutoka kwa wanafunzi na wanapozibaini, wanatazifanyia kazi . Wanafunzi walio chini kiuwezo darasani, huwa wanapaswa kusaidiwa kuinuliwa, hata wakafikia kiwango cha kuridhisha au hata ufanisi wa juu zaidi.

Kuwainua kiuwezo, ni moja ya mafanikio makubwa ambayo yatawawezesha wanafunzi hao kufanya vizuri katika masomo.

Hivi karibuni katika Mahafali ya 17 ya Kuhitimu Kidato cha Nne katika Shule ya Sekondari ya St.Mark's iliyopo Kongowe jijini Dar es Salaam, ufafanuzi wa mengi aina hiyo yaliibuliwa.

Mkuu wa Shule, Leticia Joseph, anasema shule imeshandaa mikakati ya kutoa elimu bora, ikiwamo kuwatambua walio na uwezo wa chini kimasomo, wainuke katika nafasi zao.

Anaeleza kwamba wanatambua watoto wanazidiana kiuwezo darasani, lakini wapo ambao uwezo wao inakuwa chini kimasomo na katika kuwainua kitaaluma.\

Kwa mujibu wa Mkuu wa Shule, walio na uwezo wa chini, kuna mkakati wao umeandaliwa wakaibuliwa kimasomo kwa kuwawezesha kufanya vizuri masomoni, wakafanana na wenzao.

"Ni jukumu la walimu kujua maendeleo ya wanafunzi darasani na ukifanikiwa kujua ni rahisi kuwasaidia walio chini kimasomo," anasema Leticia .

Akizungumzia mkakati mwingine katika shule yao, mbali na kuwainua kimasomo wanafunzi walio chini, anasema wameweka mkakati wa ufaulu ambapo mkakati huo umezaa matunda na ufaulu kila mwaka umekuwa mzuri kwa wanafunzi wa vidato vya pili na nne

Leticia anasema shule yao imekuwa na mafanikio makubwa katika ufaulu, ukiwa ni mwendelezo wa wanachokipata na hali hiyo kuifanya shule hiyo kuwa na matokeo mazuri kwa kila mwaka.

Anatoa mfano wa wahitimu wa kidato cha nne wanafunguliwa milango ya kujiunga kidato cha tano na wengine kuelekea vyuoni.

Anafafanua mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano mzuri wa masomo uliopo baina ya walimu na wanafunzi yanayotolewa.

Mkuu wa Shule huyo, anasema katika kipindi cha mwaka jana, wanafunzi kidato cha nne walifaulu kwa asilimia 100, huku kidato cha pili ni asilimia 99.

Anataja mafanikio mengine ambayo shule imekuwa ikiyapata kupitia mitihani, ni kuwapo walimu wa kutosha, maabara zenye vifaa vya kutosha, maktaba yenye vifaa vilivyojitosheleza. Anaongeza kuwa shule yao imeanzisha klabu za wanafunzi kujisomea hatua hiyo ni moja ya mafanikio katika kuongeza ufaulu.

Mwalimu Leticia anasema, shule imefanikiwa katika maboresho ya miundombinu, ambayo kwa watoto wa jinsia zote; wa kike na kiume .

Akitoa nasaha kwa wahitimu, anawakumbusha kuwa maadili mema waliyoyapata shuleni, yanapaswa kuendelezwa majumbani mwao, kwa kutojiingiza katika makundi yasiyofaa.

"Shule imewalea kimaadili na mnapomaliza mitihani yenu muyaendeleze mema mliyoyapata shule na sio kujiingiza katika makundi yasiyofaa ",alitamka Mkuu wa Shule, anayezungumzia vijana wake shuleni zaidi ya 70 wanatarajia kufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka huu.

# Mwananchi ailalamikia halmashauri

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWANANCHI Samweli Kyando, anayefanya biashara ya huduma ya choo, kituo cha mabasi Tukuyu Mjini, ameilalamikia Halmashauri ya Wilaya Rungwe kwa madai ya kumnyang'anya choo hicho, alichodai kukijenga tangu mwaka 1996 kwa Sh. milioni 80. Kufuatia tukio hilo, Kyando amemuomba Rais Dk. John Magufuli, aingilie kati suala hilo, ili haki iweze kutendeka.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Loema Peter, alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu suala hilo, alisema halmashauri imekichukua choo hicho kwasababu mwananchi huyo hana nyaraka zinazoonyesha ni mali yake.

"Ardhi ni mali ya serikali, kama yeye alijenga hicho choo kwenye ardhi ambayo siyo ya kwake, mmiliki wa ardhi anapoamua kuichukua anamiliki na kila kitu kilichopo juu ya ardhi," alisema Peter.

Kwa mujibu wa Kyando mwaka 1996 halmashauri hiyo ilitangaza zabuni ya kujenga na kuendesha choo katika kituo cha mabasi, katika Mji wa Tukuyu na yeye alipeleka barua ya maombi Agosti 28, 1996 na kupewa kwa makubaliano ya kujenga kwa gharama zake na kukiendesha.

"Nilijenga jengo hilo likiwa na vyoo vyenye matundu saba, wanawake matundu matatu na bafu na wanaume matundu manne, bafu na sehemu ya kuogea na vyumba vya barabara vitano kwa gharama ya Sh. milioni 80," ilieleza sehemu ya barua hiyo aliyoipeleka ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kulalamikia jambo hilo.

Alisema katika hali ya kushangaza Novemba 2017, aliandikiwa barua na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe, kwamba halmashauri haijawahi kupata kibali chochote cha kufanya ujenzi au ukarabati wa choo cha kituo cha mabasi.

"Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Rungwe inapenda kukuamuru kuondoka kwenye kukusanya mapato yatokanayo na choo cha stendi Tukuyu Mjini," imeeleza barua hiyo iliyosainiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Loema Peter.

Kyando alisema, tangu aandikiwe barua hiyo amekuwa akipewa onyo kwamba kama ataendelea kuving'ang'ania vyoo hivyo, atafunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Alisema katika kipindi chote amekuwa akiendesha vyoo hivyo na kila mwezi kutoa mapato katika halmashauri hiyo.

Alisema hapingi uamuzi wa halmashauri hiyo kutaka kuvichukua vyoo hivyo, lakini anachotaka, alipwe haki yake zaidi ya Sh. milioni 80, ambazo alizitumia kwa ujenzi wa vyoo hivyo badala ya kutumia mabavu kumnyang'anya.

"Tangu sakata hili limeanza nimekosa amani sana mara natishiwa hadi kushtakiwa kwa kesi ya uhujumu uchumi, kwa kweli namuomba Rais Dk. John Magufuli aingilie kati suala hili, ili haki itendeke," alisema.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (katikati), akiwa katika vazi rasmi la kimasai alilovalishwa na wagombea ubunge wa Jimbo la Arusha Mjini, Mrisho Gambo na Udiwani Kata ya Murieti, Francis Mbise ikiwa ishara ya upendo na heshima, kabla ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika kata hiyo, juzi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Serikali yaanika sababu kasi ya mikopo kwa wachimbaji wadogo

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

SERIKALI imesema uanzishwaji wa masoko ya madini nchini umekuwa ni moja njia muhimu itakayoongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo nchini.

Akizungumza kwenye Kongamano la Fursa za Uwekezaji na Biashara lililofanyika kwenye maonyesho ya madini na teknolojia yanayofanyika mkoani Geita, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, alisema kupitia masoko hayo wachimbaji hao wanauza madini kwa uwazi huku taarifa za mienendo ya biashara zao zikitoa fursa kwa taasisi za fedha kuwapatia mikopo.

"Tunaamini uwapo wa taarifa za mienendo ya biashara za wachimbaji wadogo kwenye masoko yetu ya madini utazisaidia sana taasisi zetu za kifedha," alisema Prof. Msanjila.

Aliipongeza benki ya NBC kwa namna ilivyojipanga kuwasaidia wachimbaji hao kupitia mafunzo ya kiutendaji na fursa ya mikopo, na kwamba imeonyesha nia ya kuwasaidia wachimbaji wadogo ili waweze kupata mikopo hususani baada ya kuwafanyia mafunzo kupitia maonyesho hayo.

Kadhalika, Prof. Msanjila aliitaka migodi yote nchini kuhakikisha inatoa ushirikiano na taasisi za fedha katika masuala ya huduma za kibenki pamoja na kuwasaidia wazabuni wa migodi hiyo kupata nyaraka muhimu zitakazosaidia taasisi za kifedha kuwapatia mikopo wanapohitaji ili kuboresha huduma wanazotoa kwa wateja wao.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, alisema hatua ya taasisi za kibenki kuanza kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo ni dalili nzuri kuelekea mabadiliko ya kiuchumi kwa wachimbaji hao pamoja na serikali kwa ujumla kwa kuwa kupitia mikopo hiyo si tu inawaongezea mitaji wachimbaji hao bali pia inaambatana na mafunzo maalumu yanayowawezesha kufanya shughuli zao kwa ubora zaidi.

"Mfano mzuri ni mafunzo yaliyotolewa na benki ya NBC kwa wachimbaji wadogo na wajasiriamali. Tafsiri yake hawa watu si tu watajengewa uwezo kifedha bali pia watakuwa na uelewa wa kutosha katika kufanya shughuli zao.," alisema Mhandisi Gabriel.

Akiwasilisha mada kuhusu uwekezaji kupitia benki katika kongamano hilo Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki kutoka Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje, aliiomba serikali itoe msukumo zaidi kwa migodi mikubwa nchini kuhakikisha inatoa mikataba ya uhakika kwa watoa huduma wake ili iwe rahisi kwa taasisi za kifedha kutumia mikataba hiyo kama dhamana ya mikopo kwa watoa huduma hao.

"Tuna huduma ya utoaji wa mikopo isiyo na dhamana kwa wazabuni wa makampuni mbalimbali ila tunachohitaji ni kuona kwamba huyu mzabuni tunaempatia mkopo anathibitisha uhalali na thamani ya zabuni yake kupitia mkataba," alifafanua.

Aliipongeza serikali kwa kusimamia vema uanzishwaji wa masoko ya madini nchini.

## Maandalizi mpango wa tatu maendeleo sasa yaanza rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango, imeanza maandalizi ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wenye dhima ya kujenga uchumi shindani utakaoongozwa na mauzo nje ya nchi.

Akifungua jana Kongamano la Wanamipango la mwaka 2020, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Doto James, alisema wataalam hao wanapaswa kutoa maoni na ushauri utakaosaidia maandalizi hayo ili nchi ipige hatua zaidi katika hadhi ya uchumi wa kipato cha kati.

"Mada za kongamano hili kwa kiasi kikubwa zimejielekeza kwenye dhima ya mpango husika zikiwa na nia ya kuainisha maeneo ambayo nchi inahitaji kutekeleza ili kufikia lengo lililokusudiwa," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema mwaka 2020/21 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, hivyo wizara imeanza tathmini ya utekelezaji wa mpango huo na matokeo yake yatakuwa msingi wa maandalizi wa mpango wa tatu.

"Wizara inatambua umuhimu wenu na nafasi yenu katika tathmini hii na pia katika maandalizi haya kwani ninyi ndiyo watekelezaji wakubwa wa miradi katika sekta, taasisi, ofisi zenu hususan kutoa takwimu zitakazosaidia tathmini husika na maandalizi ya mpango wa tatu," alisema.

Pia alitumia fursa hiyo kubainisha vikwazo wanavyokabiliana navyo kuwa ni pamoja na upatikanaji na utunzaji wa taarifa za miradi ambazo kimsingi ndizo huwezesha maandalizi ya mipango na kufanya tathmini ya utekelezaji.

"Hichi ni kikwazo kikubwa katika kuainisha hatua zilizoigwa na nchi kuitia miango yetu, hata hivyo Wizara imetengeneza mfumo wa Kitaifa wa kusimamia miradi ya maendeleo ili kutatua kero zilizokuwa zikitukabili hususan upatikanaji wa taarifa hizo kwa wakati,"alisema.

Alisema mfumo huo utakuwa na sehemu zote za mzunguko wa miradi ikiwamo uibuaji, ugharamiaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini, utoaji taarifa na ufungaji wa mradi baada ya utekelezaji kukamilika.

Pia alisema kwa kutambua mchango wa wanamipango serikali inaandaa mfumo ambao utakuwa na taarifa za wanamipango wote kwa lengo la kuwatambua na kuwa na mikakati madhubuti ya kuilea kada hiyo.

Naye Kamishna wa Mipango ya Kitaifa ya Wizara hiyo, Dk. Nicolaus Shombe, alisema kongamano hilo limeitishwa kwa lengo la kupata mawazo ya wadau wa mipango kwa ajili ya kufanya tathmini ya mpango wa pili na kuandaa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa 2021/22- 2025/26.

# UN Women kukutanisha wadau jinsia

**Na Frank Maxmillian,** TUDARCo

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linalojishughulisha na masuala ya wanawake (UN Women), limesema kuwa wanawake vijana wana wajibu wa kuchaguliwa kama viongozi na watoa maamuzi na kuchangia usawa wa kijinsia.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na UN Women, ilisema zaidi ya washiriki 100 wakiwamo viongozi wa serikali, wanaharakati wa jinsia, kundi la wanaume na mitandao ya wanawake wa sekta binafsi na umma, watajadili mpango utakaosaidia wasichana wadogo kushika nafasi za uongozi na kushiriki katika ngazi za uamuzi.

Mazungumzo hayo yanafanyika ikiwa ni kuadhimisha kampeni ya usawa wa kikazi utakaosaidia kutambua haki za wanawake wakati ujao, ikiwa ni miaka 25 ya jukwaa la utekelezaji wa azimio la Beijing.

Mashirika ya utetezi wa jinsia nchini yatakayoshiriki ni Msichana Initiative, Plan international, Mtandao wa Viongozi wa Wanawake wa Afrika (AWLN), Ubalozi wa Ufaransa na Kikundi cha Ushauri cha jamii ya wanawake cha umoja wa mataifa (CSAG). Kampeni ya usawa wa kizazi ni ya Umoja wa Mataifa ya wanawake duniani iliyozinduliwa mwaka 2019 ili kujenga msukumo wa maadhimisho ya 25 ya jukwaa la utekelezaji la Beijing na kuunda fursa ambazo zitakusanya vizazi vijavyo vya wanaharakati wa haki za wanawake na watetezi wa usawa wa kijinsia.

"Tunafanyakazi kuhakikisha kuwa mazingira ya kutunga sheria yanaongeza ushiriki wa wanawake na uwakilishi katika nafasi za uamuzi sekta zote. Kupitia ushirikiano na mashirika kama UN Women, tunaunga mkono juhudi za kubadilisha kanuni za kijinsia ambazo zinawabagua wanawake wachanga wakati wa uchaguzi na uteuzi wa viongozi," alisema Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg.

Katika mahojiano yake jana, Mwakilishi wa UN Women nchini, Hodan Addou, alisema maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 10 mwaka huu, yameonyesha jinsi shirika hilo litafanyakazi na wadau mbalimbali ikiwamo serikali katika kujadili vikwazo zinavyowakabili wanawake nchini. Mwanzilishi na Mkurugenzi wa Msichana Initiative, Rebecca Gyumi, alisema: "Wanawake na wasichana wachanga wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na changamoto nyingi kwa sababu ya ukosefu wa usawa unaotokana na tabia za kijamii kama vile unyanyasaji wa kijinsia na vitendo vingine hatari."

Naye, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake, Zlatan Milisi, alisema wanaume na wavulana wanajukumu la kusaidia uwezeshaji wa wanawake na wasichana kwa kuwa wote wastahili kufaidika na Tanzania inayolingana na jinsia.

# Vijana 200 kimataifa kujadili amani

**Na Romana Mallya**

VIJANA zaidi ya 200 kutoka nchi mbalimbali barani Afrika wanatarajiwa kukutana jijini Arusha kujadili utafiti wa Umoja wa Mataifa (UN), unaohusu mustakabali kama dunia kuhusu ushiriki wao wa kutunza amani ya taifa.

Ofisa Habari wa Kituo cha Habari UN, Didi Nafisa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano kivuli ambao utafanyika kwa siku nne jijini humo kuanzia Jumanne ijayo.

Didi alisema mkutano huo unaratibiwa na Asasi ya Vijana Umoja wa Mataifa Tanzania (YUNA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Mashirika Umoja wa Mataifa Tanzania.

Alisema vijana watakaoshiriki mkutano huo watatoa mawazo yao kama wanachama wengine na kuwasilishwa Makao Makuu ya UN.

Alisema mwaka huu UN inatimiza miaka 75, hivyo wanaungana na asasi ya YUNA ili kutoa fursa kwa vijana kuzungumzia utafiti huo ambao unaendelea hivi sasa kitaifa na kimataifa.

Mratibu wa mkutano huo, Philemon Mweleka, alisema miongoni mwa mambo yatakayodiliwa na vijana ni pamoja na wajibu wao kwenye masuala ya afya ya uzazi na upingaji ukatili wa kijinsia.

Pia, watazungumzia maarifa ya vijana kufanya kazi zenye kuleta ajira, ushiriki wao kwenye utunzaji wa mazingira ambao unaweza kuwaletea kipato na wajibu wao katika kutunza amani ya taifa.

Alisema mkutano huo wa 23, unawahusisha vijana wa Tanzania Bara na Visiwani na wa kutoka nchi mbalimbali barani Afrika.

"Tunaufanyia Arusha kwa sababu zipo changamoto za kijamii kwenye sekta ya afya, elimu, uchumi na wanawake na kijinsia tumezibaini," alisema.

Akizungumzia ushiriki wa vijana kwenye uchaguzi mkuu, Katibu Mkuu wa YUNA Tanzania, Kelvin Edward, alisema wameona vijana wengi wamejitokeza kuwania nafasi ngazi mbalimbali za kiuongozi na kushiriki mchakato wa uchaguzi.

Alisema mkutano wa Arusha umelenga pia kuwakumbusha vijana kuwa wana nafasi ya kuleta mabadiliko.



Mkazi wa Kata ya Kwembe Mpakani Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, akichota maji kwenye kisima jana, ambapo ndoo moja ya maji huuzwa kwa 200/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wadau wa korosho kuuza mfumo stakabadhi ghalani

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WADAU wa korosho mikoa ya Ruvuma, Njombe na Mbeya wamekubaliana kuanza kuuza zao hilo kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu wa mwaka 2020/2021 kuanzia Oktoba 22, mwaka huu.

Wadau hao pia wamekubaliana kuuza korosho zao kwa kutumia utaratibu wa minada ambayo itafanyika kupitia njia ya mtandao ambao utatoa nafasi kwa wanunuzi wa nje ya nchi kutuma barua za maombi ya kununua korosho (TMX) na sanduku ambalo pia litatumika kuweka barua za wanunuzi waliopo nchini kwa ajili ya ushindani wa kununua korosho hizo.

Wadau hao walifikia makubaliano hayo kwenye kikao cha mkutano wa tasnia wa korosho kilichofanyika mjini hapa na kwamba wamepanga kuanza tarehe hiyo, ili kutoa nafasi kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima (AMCOS) kukamilisha maandalizi na kuanza kukusanya korosho kutoka kwa wanachama wao na kuzisafirisha hadi kwenye maghala ya minada.

Akitangaza taarifa ya maazimio hayo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Chrisina Mndeme, alisema pamoja na mambo mengine serikali ina amini kuwa maandalizi yatafanyika na kukamilishwa mapema ikiwa ni pamoja na kupanga safu za wafanyakazi waaminifu katika vyama vyote vya msingi ili kuwaondolea usumbufu wa kupoteza mazao ya wakulima.

Alisema serikali imejipanga kwa ajili ya usimamizi hivyo itakuwa macho kuangalia mwenendo wa utekelezaji wa shughuli zote za mauzo ya korosho za wakulima na kwamba kiongozi yoyote atakayekuwa na nia mbaya ya kuhujumu mfumo, kuiba mazao au fedha za wakulima ajiandae kuchukuliwa hatua za kisheria.

Taarifa iliyotolewa na Meneja wa Bodi ya Korosho Tanzania tawi la Tunduru, Shauri Mokiwa, ilisema kuwa Chama Kikuu cha Wakulima Tunduru (TAMCU), kilikisia kuzalisha kilo 30,000,000, lakini kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa katika msimu huu makisio ya uzalishaji yameshuka hadi kilo 25,000,000 ikiwa na ongezeko la asilimia 1.5 kulinganishwa na uzalishaji wa kilo 24,625,824 za msimu wa 2019/2020.

Mwenyekiti wa TAMCU, Hashimu Mbalabala, alisema kuwa tayari kuna magunia 170,000 na tayari mzabuni wa kusambaza magunia ameahidi kukamilisha uletaji wa magunia 130,000 kati ya 300,000 yalipopangwa kutumika katika kipindi cha msimu wa Septemba 30, mwaka huu, ili kupunguza adha kwa wakulima.

# Ndikilo ataka viwanda viajiri walinzi wenye mafunzo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo, ametoa angalizo kwa wamiliki wa viwanda vilivyopo katika wilaya hiyo kuzingatia walinzi wanaowapatia ajira, wawe walioopata mafunzo.

Ntemo aliyasema hayo mjini hapa, alipokuwa katika ziara ya siku moja na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, kukagua baadhi ya viwanda katika wilaya hiyo kikiwamo cha kutengeneza mabasi ya abiria cha BM.

Alisema, ofisi yake itaendelea kutoa ushirikiano kwa wawekezaji itakapohitajika, lakini wanatakiwa kuzingatia kampuni zinazopatiwa kazi za ulinzi iwe kwa wale waliopitishwa kwenye mafunzo.

Akiwa katika kiwanda hicho cha BM kinachomilikiwa na Jonas Nyagawa, Mkuu wa mkoa alisema anajivunia kuwa na kiwanda kama hicho katika mkoa wake ambacho hakuna mwekezaji mwingine aliyewekeza nchini.

Kuhusu tatizo la barabara kufika katika kiwanda hicho na vingine 25 vilivyojengwa katika eneo la Zegereni, Ndikilo aliahidi ujenzi wa kiwango cha lami kurahisisha usafirishaji wa malighafi za kiwandani na bidhaa zinazotengenezwa.

Alisema, tayari upembuzi yakinifu wa barabara hiyo umeshafanyika kwa kilomita 12 kutoka Visiga hadi eneo la Viwandani Zegereni na katika bajeti ya 2020/2021 kilomita moja, itaanza kujengwa kwa lami.

Alisema gharama za kuagiza basi la abiria nje ya nchi ni zaidi ya milioni 400 na ukinunua katika kampuni hiyo ya BM ni Sh. milioni 250 hivyo uwepo wa kampuni hiyo, utasaidia wafanyabiashara kuokoa fedha zao.

Mkurugenzi wa Kampuni ya BM Motors, Jonas Nyagawa, alimweleza Mkuu huyo wa Mkoa kuwa kiwanda hicho cha kuunganisha magari kitakuwa na uwezo wa kuunganisha mabasi 60 kwa mwaka. Nyagawa alisema kampuni yake itakuwa na uwezo wa kutoa ajira 40 za moja kwa moja na 80 zisizo rasmi na kwa sasa asilimia 60 ya malighafi anazipata kutoa nje ya nchi na 40 pekee ndani ya nchi.




Mafundi wakijenga kituo cha mabasi ya mwendokasi katika mradi unaoendelea wa ujenzi wa miundombinu ya mabasi hayo katika barabara ya Kilwa eneo la Mbagala Zakhem, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwarobaini wa kero ya maji wapatikana

**Na Neema Hussein,** KATAVI

KUPATIKANA kwa chanzo cha maji kinachojulikana kama Ikolongo 2, kimetajwa kutatua changamoto ya maji inayowapata wakazi wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi.

Akizungumza baada ya kukagua chanzo hicho Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, alisema wanatarajia kupunguza changamoto ya maji kwa kiasi kikubwa endapo watafanikiwa kuyatoa kwenye chanzo hicho na kuyapeleka kwenye tangi kubwa linalojengwa katika Kijiji cha Mapinduzi kisha kuyasambaza kwa wananchi.

Alisema kazi ya kuyatoa maji hayo katika chanzo hicho imeshaanza na tayari yamefika Mpanda Mjini zimebaki kilometa tatu kati ya 25 kutoka eneo husika ili kuyafikisha kwenye tangi hilo.

Homera alisema changamoto iliyokwamisha maji hayo kufika kwa haraka ni kutokana na deni la zaidi ya Sh. milioni 455 analodai mkandarasi.

Hata hivyo aliahidi kufikisha taarifa za deni hilo kwa Waziri wa Maji ili aweze kusaidia kulipwa ili wananchi wafaidike na maji hayo. Alisema uwezo wa chanzo hicho ni zaidi ya lita milioni tatu za maji na Wilaya ya Mpanda inahitaji maji lita milioni 1 hadi Sh. milioni 1.5, hivyo kukamilika kwa mradi huo kutatatua kabisa changamoto hiyo. Baada ya ukaguzi huo Homera alizindua kisima cha maji katika Kijiji cha Milala ikiwa ni miongoni mwa mradi wa visima 15 unaosimamiwa na Mamlaka ya Maji Mpanda (MUWASA). Aidha, Homera na Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Yusuph, walishiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la kisima hicho ikiwa ni ishara ya utunzaji wa mazingira katika kijiji hicho.

# Wajipanga kukusanya chupa 2,700 za damu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JUMLA ya chupa za damu 2,700 zinatarajiwa kukusanywa mkoani Kagera

kwa kipindi cha wiki moja kuanzia Septemba 21 hadi leo kwa nchi nzima.

Akizungumza na Nipashe mshauri wa kitengo cha damu salama katika mkoa wa Kagera, Bashweka Amos alisema kuwa ili kuhakikisha malengo yao yanatimia kila halmashauri imewekewa lengo la kukusanya chupa 300 katika wiki moja ya uhamasishaji.

"Ipo timu ya wataalamu wanaoendelea na kazi hiyo na inasubiriwa siku ya mwisho ili kuona kama malengo yetu yametimia au hayajatimia," alisema.

Aliongeza kuwa kituo cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Bukoba kinahitaji wastani wa kati ya chupa 200 hadi 250 kwa mwezi.

Aidha, alisema mbali na kampeni hiyo kila siku wanaendelea na zoezi la kuomba watu wajitokeza kujitolea damu na kuwa hawawezi kusubiri kampeni tu wakati damu kila kukicha inahitajika.

# 'Urejelezaji vyuma chakavu kuongeza tija viwandani'

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema kuwa urejelezaji wa taka na vyuma chakavu utachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa malighafi za viwanda na kupunguza gharama za kuigiza malighafi hizo nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita Watanzania wameitika vizuri biashara ya kuchakata vyuma chakavu na hivyo kuongeza upatikanaji wa malighafi viwandani.

"Mfumo wa urejelezaji wa vyuma chakavu na taka za aina nyingine katika kipindi cha miaka mitano iliyopita umeleta mafanikio makubwa kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja, lakini pia umeongeza kasi ya upatikanji wa malighafi katika viwanda vyetu vya ndani,'' amesema.

Alisema kuwa uagizaji wa malighafi kutoka nje ya nchi umekuwa ni gharama kubwa kwa wenye viwanda na malighafi hutumia muda mrefu kufika nchini, kasoro ambazo huzorotesha utendaji wa kazi viwandani.

"Serikali ya awamu ya tano imekuwa ikitekeleza azma yake ya ujenzi wa viwanda, tunahitaji kuunga mkono jitihada hizo kwa kuhakikisha panakuwapo na uhakika wa malighafi za ndani badala ya kuagiza kutoka nje kwa gharama kubwa na muda mrefu,'' alisema Dk. Gwamaka.

Aidha, Dk. Gwamaka amezitaka halmashauri zote nchini kutengeneza utaratibu mzuri wa namna ya kukusanya taka, ili kurahisisha ukusanyaji wa vyuma chakavu na taka zingine ambazo zinaweza kurejelezwa katika viwanda hapa nchini.

# Mgombea atangaza neema huduma za jamii

**Na Happy Severine, SIMIYU**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Bariadi mkoani Simiyu, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Andrew Kundo, ameahidi kutatua changamoto ya huduma za afya, barabara, maji na elimu kwa wananchi wa kata ya Ikungu-lyabashashi na Gudui.

Mhandisi Kundo alisema kuwa endapo atachaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo, atashughulikia kero hiyo ili wananchi waweze kuishi vizuri.

Mgombea huyo alitoa ahadi hiyo mbele ya umati wa wananchi waliofika kwenye mkutano wa hadhara wa kampeni zinazoendelea katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo.

Katika Shule ya Msingi ya Mwahalaja mgombea huyo aliahidi kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ambavyo vinahitaji zaidi ya mabati 100.

Katika mkutano huo, Kundo alimwombea kura mgombea wa urais kupitia CCM, Rais John Magufuli.

# Aahidi kupeleka maendeleo Msasani

**Na Mary Geofrey**

MGOMBEA wa udiwani kupitia CCM Kata ya Msasani, Luca Neghesti, amewaomba wananchi kumchagua ili awaletee maendeleo ikiwamo ya kuwaunganisha na huduma za afya za CHF.

Aidha, amesema endapo atapewa ridhaa hiyo pia atasimamia utoaji wa mikopo pamoja na elimu ya fursa za kibiashara, ili kuwainua wananchi wa kata hiyo.

Neghethi aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kampeni zake za kuwania nafasi hiyo zilizofanyika mapema wiki hii na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama hicho, akiwamo aliyewahi kuwa Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Salum Londa.

Alisema Kata ya Msasani inahitaji mtu mchapakazi na endapo wananchi watampa ridhaa hiyo, atahakikisha anashirikiana nao kwa kila hali kutatua changamoto zinazowakabili ikiwamo changamoto ya mitaro, ukosefu wa soko na kusimamia ujenzi wa soko jipya la samaki la Msasani.

Aliahidi kuwa pamoja na mambo mengine atahakikisha anasimamia ipasavyo suala la ukusanyaji taka katika kata hiyo kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa ili magari ya uzoaji taka yawe yanafanya kazi kwa utaratibu mzuri na kuangalia namna ya nyingine ya uchakataji wa taka ili kuboresha mazingira.

Kuhusu ajira kwa vijana, mgombea huyo alisema atatengeneza mfumo maalumu utakaowatambua vijana hao ili kurahisisha mpango wa kuwatafutia kazi katika maeneo mbalimbali ikiwamo viwandani.

# Wajasiriamali waomba maboresho vitambulisho vyao

**Na Happy Severine, BARIADI**

BAADHI ya wajasiriamali wilayani Bariadi mkoani Simiyu, wamesema

vitambulisho vya wamachinga walivyopatiwa vimekuwa msaada, huku

wakiomba ifanyiwe maboresho kwa kuongezwa jina na picha ya wahusika.

Aidha, wameongeza kuwa awali kabla ya zoezi la vitambulisho walikuwa wakitumia pesa nyingi kulipia ushuru wa halmashauri hali iliyopelekea baadhi yao kushindwa kuendelea na biashara zao na kudondokea katika mikopo.

Wafanyabiashara hao walisema hayo jana wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, katika mgodi wa Gasuma uliopo wilayani Bariadi.

Walisema vitambulisho hivyo vimepunguza usumbufu waliokuwa wakiupata pamoja na ulipishwaji holela wa ushuru wa kila siku.

Ramadhan Kakwamba mchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu alieleza kuwa kabla ya utaratibu wa utoaji wa vitambulisho hivyo wajasiriamali wengi walikuwa wakinyanyaswa na askari mgambo na wakati mwingine walikuwa wakilazimika kutoa rushwa ili wasisumbuliwe.

Dk. Edward Ihoyelo, alisema vitambulisho hivyo vimeondoa kero walizokuwa wanakutana nazo wafanyabiashara hususan wadogo.

Aliongeza kuwa ni vema serikali ikafanya maboresho katika vitambulisho hivyo kwa kuviwekea majina na picha cha wahusika ili kuepuka kuibiana.

Kwa upande wake Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Elias Stephano, alisema kwa mwaka 2020 wamepokea vitambulisho 9,000 ambapo awamu ya kwanza walipokea 1,500 na awamu ya pili 7,500 huku akiongeza kuwa mwitikio wa wananchi kuchukua vitambulisho hivyo ni mkubwa na wengi wanasema vimewapunguzia adha ya ushuru wa mara kwa mara. Akizungumza na wafanyabiashara soko kuu na la mji wa Bariadi, Festo Kiswaga, amewataka wajasiriamali kupuuza maneno ya uzushi dhidi ya vitambulisho hivyo na wanaopotosha wameishiwa hoja za kwenye majukwaa.

# World Vision wamwaga bil. 2.3/- kukuza elimu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

SHIRIKA lisilo la kiserkali la World Vision Tanzania, limetenga kiasi cha Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya kukuza kiwango cha elimu kwa wanafunzi wa darasa la awali mpaka la tatu katika shule za msingi zilizopo kata za Kilago na Iyenze Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga.

Fedha hizo zimetolewa kwenye mradi wa kukuza stadi za usomaji kwa wanafunzi hao ili kuondoa tatizo la wanafunzi kuhitimu elimu ya msingi wakiwa hawajui kusoma na kuandika.

Hayo yalibainishwa jana wilayani Kahama na Meneja wa Kanda, John Massenza, wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, ambapo alisema mradi wa kukuza stadi za usomaji kwa wanafunzi hao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 na ulianza tangu mwaka 2017 na unatarajia kukamilika ifikapo mwaka 2027.

Alisema kuwa, shirika limetenga kiasi cha Sh. bilioni 2.3 za kukuza elimu katika kata za Iyenze na Kilago na kutokomeza janga la wanafunzi kuhitimu elimu ya msingi wakiwa hawajui kusoma na kuandika.

Mradi huo unatarajia kuwafikia wanafunzi zaidi ya 20,000, wazazi na walimu wa shule hizo zaidi ya 45,000.

"Kabla ya kuanza kwa mradi huu, tulifanya tathmini shule zote za msingi zilizopo Halmashauri ya Mji wa Kahama, tulibaini shule zilizopo Kata ya Iyenze na Kilago ufaulu wake uko chini kwa asilimia 15.

Alisema kati ya wanafunzi 100 wanahitimu masomo, wanafunzi 15 ndio wanaojua kusoma na kuandika vizuri," alisema Massenza.

Akizungumza kwa niaba ya walimu wa shule za msingi za kata ya Kilago na Iyenze, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Iyenze, Neema Chiloloma, alisema, uwepo wa mradi huo umeongeza uelewa kwa wanafunzi wa awali na darasa la tatu na wengi wao kwa sasa wanajua kusoma ukilinganisha na kipindi cha nyuma.




Mtaalamu wa Kilimo wa Taasisi ya Maua Mazuri, Steven Tumaini (kulia), akiwapa maelezo namna ya kuandaa mbegu ya mgomba unaozalisha ndizi kwa wingi maofisa wa Benki ya NMB, kwenye kongamano la wafanyabiashara wadogo na wakati, lililoandaliwa na benki hiyo, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgombea CHADEMA ataka ushindi wa haki

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Vwawa mkoani Songwe kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Fanuel Mkisi, amesema atamsindikiza Dodoma kwenda kuapishwa bungeni mgombea wa CCM katika jimbo hilo, Japhet Hasunga kama atashinda ubunge kwa haki.

Hasunga ni mbunge aliyemaliza muda wake ambaye anachuana na Mkisi kwa mara ya pili katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza jana na wananchi wa kata ya Kilimapimbi kwenye mkutano wa kampeni, alisema safari hii endapo atakusanya matokeo katika vituo vya kupigia kura ikaonekana ameshinda na Tume ya Taifa itamtangaza bila kuweka figisu.

"Endapo mwenzangu Japhet Hasunga (mgombea wa CCM) atakuwa ameshinda kwa haki nitamuunga mkono na nitamsindikiza Dodoma kuapishwa, maana sisi sote ni wana Vwawa tunajenga nyumba moja hatutakiwi kung'ang'aniana fito, atakayeshinda tutamsapoti ili aweze kutimiza ahadi zake," alisema.

Mkisi akizungumza kuhusu huduma za afya, aliwaahidi wananchi kuwa mara tu atakapochaguliwa atakwenda kuonana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili asaidie kuleta wahudumu wa afya wauguzi na madaktari katika zahanati ya Kilimapimbi.

Alisema zahanati hiyo ambayo ilijengwa kwa mamilioni ya fedha zikiwamo zilizochangwa na wananchi, ni miaka mitano sasa haina wahudumu wa afya na hivyo wananchi kukosa huduma za afya.

Kuhusu michango, alisema akichaguliwa wananchi hawatatozwa michango zaidi ya shilingi elfu 3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo zitakuwa zinatolewa kwa awamu.

Mkisi alisema inashangaza hivi sasa wananchi wanatozwa michango mikubwa kuanzia elfu 20 bila kujali kuwa kipato chao ni kidogo.




RC Ndikilo akagua uwekezaji mabilioni viwanda vya Kibaha




TARI: Zabibu zetu 'zimefunika' duniani



# Choroko yalimwa kisasa, yatwaa chati kupendwa, zao la biashara

**Na Renatha Msungu,** Dodoma



Mkurugenzi wa Kanda wa taasisi ya Vegetable Centre, Dk. Gabriel Rugalema, akionyesha mbegu za choroko zinazohifadhiwa maabara. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

WORLD Vegetable Centre ni taasisi inayojishughulisha na utafiti wa mbegu za mboga, pia inafundisha wakulima kuongeza thamani ya zao la choroko ambayo sasa ni neema kwa kipato cha wakulima.

Inachukua sura kufananisha na kile cha mboga za majani, ambacho uelewa wake uko nchini.

Asasi hiyo imeanzisha shamba darasa la kufundishia wahitaji wa kilimo cha mboga na juhudi sasa ikizama kwenye choroko, kwani wakulima wengi hawakujua thamani yake, lakini baada ya uelewa huo inatumika kuwa ao la biashara kwa wakazi mbalimbali nchini.

Aidha, choroko imekuwa zao la thamani baada ya kuanza kutumiwa na wajawazito, ukiwa mbadala wa kunywa vidonge aina ya dawa mojawapo na kupata virutubisho mbadala.

Kinachofanyika ni kuongezwa thamani ya choroko, hata kupanua kipato kwa mkulima anayezalisha.

Thamani mojawapo ni kwamba, inaweza kumpatia mtu kipato na kubadili aina ya mapishi, kutengeneza bidhaa kama unga zinazonunuliwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Choroko zinaweza kupikwa katika aina tofauti kutegemea na makundi ya watu waliopo, kama unga wa kupika bidhaa zinazoweza kuuzwa, ikiwamo keki.

Orodha zina bidhaa za milo kama keki biskuti, sambusa, uji, supu ya choroko, mseto wa choroko, kande na kababu.

Vitu hivyo huuzika sana katika baadhi ya mikoa, ambako asasi ya World Vegetable imefika kutoa ujuzi wa kuongeza thamani ya ili waletee faida wakulima.

Wengi kwa sasa wanalima kwa sababu wamejua kuongeza thamani yake, pia kuitumia kama mboga.

Hadi sasa wakulima wengi wanufaika nayo, tofauti na awali hawakujua thamani. Hivi sasa umma wa wakulima wanalifanya zao la biashara.

Mtafiti wa mbegu za mboga, Jeremaya Sigalla, anaiambia Nipashe kuwa choroko ilikuwa inadharauliwa, kwa sababu ya kutojulikana thamani yake.

Sigalla anasema wakulima wengi baada kufundishwa thamani ya zao hilo na wanalifanya la biashara, wakiwa na ujuzi sahihi.

"Imekuwa hivyo sasa, choroko zimekuwa sana na wakulima wameelewa uthamani wake,"anasema Sigalla.

Anasema wakulima wa zao hilo, wanakiona kipato pindi zao linapoingia sokoni kwa ajili ya kufikisha maeneo mbalimbali, uelewa ukiwafikia wote wenye nia ya kuzalisha, baada ya darasa kamili kuwafikia.

Mtafiti huyo anasema choroko imepata kichocheo kikubwa kwa wakulima kuiendeleza, kivutio kikiwa thamani wanayoiona sasa.

Sigalla anafafanua: "Kuna mazao watu wanayadharau, lakini yana faida kubwa sana yakilimwa."

Anaeleza, kwa ajili ya kuwainua wakulima kuwafundisha namna ya kuthamanisha zao hilo na kutoa bidhaa mbalimbali zinazouzwa hata kuwaingizia kipato.

Anasema, katika maonyesho ya Nanenane, walifanya kazi kubwa ya kuzisemea Choroko huku wakiwaonyesha bidhaa zilizotengenezwa kwa choroko.

Mkurugenzi wa Kanda wa Kituo hicho, Dk Gabriel Rugalema, anasema kituo kinaahidhi mbegu bora zinazotumika kuzipanda ili zilete tija.

Mkurugenzi huyo, anasema wana mpango wa kuwafundisha wakulima kuendesha kilimo cha mboga, kwa sababu kina manufaa makubwa nje na ndani ya nchi.

Anasema wakulima wakiendesha kilimo vizuri, basi kitawaidia kupanua wigo wa biashara zao.

Katika ghala lao, wanaweka mbegu ambazo watu huja pale na kuchukua kwa ajili ya kwenda kupanda.

Anasema ghala hilo linauwezo wa kuhifadhi mbegu kwa muda mrefu, ili zisiharibike na wakulima kuzitumia kupanda bustani za mboga, wanazotumia kama biashara ya kujikimu.

Anaesema vijana wamepata mwamko kutokana na uelewa wa watafiti wa kituo hicho .

Mkulima wa bustani ya mboga, Agness Mallya, anasema hivi sasa analima choroko, kama zao la biashara na matumizi ya nyumbani.

Anafafanua kuwa zao hilo ni muhimu sana kwa sababu likiongezwa thamani hutumika kufanya vitu mbalimbali.

"Tunawashukuru World vegetable Center kwa kusaidia kuinua wakulima tunaamini hawatuacha katika kuendeleza kilimo na kuinua kipato chetu, "anasema Agness.

Inaaelezwa kilimo cha mboga kina faida kubwa, kwa sababu jamii inaitumia majumbani.

BIASHARA

# TARI: Zabibu zetu 'zimefunika' duniani

## • Sifa kuu mvinyo matunda, viungo • Aina tano zinasukwa katika utafiti

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

ZABIBU ni miongoni mwa mazao yaliyopewa kipaumbele mkoani hapa na tafiti zinaonyesha, kwamba Dodoma ndio maalim pekee duniani, zabibu zinavunwa mara mbili kwa mwaka.

Uzalishaji wake umeendelea kuongezeka na kwa mujibu wa takwimu zilizoko, ni kwamba imepanda kutoka tani 8,368 mwaka 2011/12 hadi tani 16,637 katika msimu wa kilimo 2018/19, Ni ongezeko la asilimia 99.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini(TARI), inasema Tanzania ina fursa kubwa ya kuzalisha zao hilo kutokana na hali yake ya hewa kukubalika katika uzalishaji na ukuaji kwenye baadhi ya mikoa.

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Makutupora, Dk.Cornel Massawe, anasema ubora wa zabibu hiyo kusifika duniani, unatokana na kuwa na kiwango cha sukari cha kutosha anataja sababu ni kuwapo saa 12 za jua kuwapo.

"Utafiti umeonyesha kwamba, maeneo ya nyanda kame za Tanzania, ikiwamo Dodoma yanakuwa na nishati ya jua ya muda mrefu na kufanya zabibu kuwa na sukari ya kutosha.

"Inapochakatwa kwa ajili ya kutengeneza mvinyo, inakuwa na kilevi cha kutosha na hakuna haja ya mtengenezaji kuongeza sukari au kuweka spiriti na inafanya mvinyo na zabibu kuwa bora duniani," anafafanua.

"Kwenye maeneo ambayo zabibu haina sukari ya kutosha wanalazimika kuchukua spiriti kuongeza ili kufikia kiwango cha kilevi lakini zabibu ya Dodoma ni miongoni mwa zabibu bora duniani na inaongoza Kusini mwa Jangwa la Sahara, tunaringia zabibu ya Dodoma," anasema.

Aidha, anasema kadri mchuzi wa zabibu unavyokaa ndivyo ubora unaendelea kuongezeka hata ikikaa zaidi ya miaka mitano.

Dk.Massawe anasema kwa sasa kituo hicho kinatoa mafunzo ya namna ya kuchakata zabibu, ambapo zamani wakulima walikuwa wakitegemea kuuzia viwanda, lakini vinanunua mzigo mkubwa na kushindwa kuchakata kwa wakati.

"Walijikuta zabibu yao ikioza shambani, lakini baada ya kupata mafunzo, wakulima nao sasa hivi wanachakata zabibu yao na kuuzia viwanda kama juisi na imesaidia kuongeza thamani

"Wakulima wengi sasa wanajua kuchakata na kusindika, na wanatengeneza wine kwa ajili ya familia zao, Dodoma tuna viwanda viwili vikubwa na vingine sita vinavyotambulika kisheria kwa ajili ya uchakataji zabibu, mafunzo yamekuwa msaada kwa wakulima," anafafanua

Dk. Massawe anasema uchakataji huo umekuwa na faida, kwani wakati kilo moja inauzwa Sh.1,200 mkulima anatumia kilo mbili zenye thamani ya Sh. 2,400 kuchakata zabibu anayoitengeneza mvinyo na kuuza kwa Sh.8,000.

"Suala la kuongeza thamani kwa kutengeneza mchuzi wa zabibu ni sehemu ya tija kwa wakulima," anasema.



Baadhi ya wakulima wa zabibu, kijijini Matumbulu, wakiwa wamebeba kreti za zao hilo baada ya kuvuna. **PICHA ZOTE: AGUSTA NJOJI.**

> **"Tunatakiwa kuwa na mbegu za kutosha tunapohamasisha kilimo, jukumu hili lipo kwa TARI ambapo inaendelea kutafiti na kuzalisha mbegu ili kuongeza uzalishaji wa zao la zabibu.**



Mkulima wa zabibu, Daniel Ngoima wa Kijiji cha Matumbulu, Dodoma, akivuna zao hilo shambani kwake.

### MBEGU

Akizungumzia kuhusu mbegu, Mkurugenzi huyo anasema kulikuwapo mbegu za kutosha ndani ya nchi, lakini tatizo likawa uzalishaji mdogo.

"Kutokana na hali hii, mkakati tulio nao kwenye hizi mbegu zilizopo nchini ambazo tumefanyia utafiti kwa sasa zipatikane kwa kiasi cha kutosha kukidhi mahitaji, tumeingia kwenye mpango wa kuhakikisha tunapanua wigo wa mbegu nchini,"anasema.

Anabainisha kuwa, shughuli za kituo hicho zinalenga katika kutekeleza programu ya kuendeleza kilimo nchini (ASDP II), ambayo wamejikita katika eneo la kuzalisha kwa tija na faida kwa wakulima.

"Sisi kama kituo katika kuhakikisha tumeyaweza hayo, tunaelekeza nguvu katika kuendesha tafiti zaidi katika zao la zabibu, lakini zaidi tunahakikisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora.

"Tunavyosema mbegu bora, ni zile zenye vigezo na zinazotakiwa na mkulima ambayo inakuwa na tija ya kutosha, ukinzani wa mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame au mafuriko, ukinzani na magonjwa,"anafafanua Dk. Massawe.

Mkurugenzi huyo anasema zabibu inayopendwa na wateja ina sifa kuu tatu inayolimwa kwa ajili ya mvinyo, matunda na viungo.

"Sisi nchini tuna aina mbili za mbegu ya zabibu ambazo zimefikishwa kwa wakulima na zote ni za kutengeneza mvinyo, lakini sisi kama kituo bado tuna aina tano za mbegu ambazo zipo kwenye utafiti za mwisho kwa ajili ya kupatikana kwa wakulima," anaeleza.

Anazitaja aina hizo ni mbili za mvinyo kwa ajili ya matunda na aina moja ajili ya viungo akitoa ufafanuzi: "Katika jitihada za kupanua wigo wa mbegu nchini tumeshirikiana na wenzetu wa Afrika Kusini, ambao wametupatia aina 13 za mbegu zote ni kwa ajili ya mvinyo na zipo kwenye mafungu mawili nyeupe na nyekundu."

Anasema nia yao baada ya mbegu hizo kufika nchini, ni kwamba wataziweka kwenye kituo cha utafiti na kuangalia zinazohimili hali ya hewa ya Tanzania na kupelekwa kwenye maeneo yanayolima zabibu nchini.

"Tunavyochukulia kwa sasa, maeneo yanayolima zabibu kwa wingi nchini ni wilaya ya Bahi, Dodoma na Chamwino. Hata hivyo, tafiti zilizofanyika zinaonyesha zabibu inaweza kustawi katika maeneo mengi ya Tanzania kuanzia Ruvuma, Mara, Tabora, Kilimanjaro, Tanga na Singida,"anasema.

Anaitambulisha hatua hiyo, inawapa matumaini kwamba mikoa inaweza kulima zabibu kwa kiwango cha juu.

### MIKAKATI WIZARANI

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, hivi karibuni akiikabidhi TARI matrekta kwa ajili ya kazi ya kuongeza uzalishaji mbegu za mazao mbalimbali na serikali imeiona zabibu kuwa moja ya mazao hayo.

"Mahitaji ya zabibu kwa sasa ni makubwa kutokana na ujenzi wa viwanda vya kuchakata mvinyo na matumizi mengine mengi" anasema. Anafafanua kuwa, ujenzi wa viwanda vya zabibu unachangia ongezeko la ajira kitaifa, hivyo kuchangia uchumi wa nchi nja kuongezea thamani.

"Tunatakiwa kuwa na mbegu za kutosha ili tunapohamasisha kilimo, jukumu hili lipo kwa TARI ambapo inaendelea kutafiti na kuzalisha mbegu ili kuongeza uzalishaji wa zao la zabibu,"anasema.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, anawataka wawekezaji kujenga viwanda vingi vya kuchakata zabibu kwa kuwa hutumika kutengeneza malighafi nyingi.

Akitembelea mashamba ya zabibu yaliyopo eneo la Mpunguzi Dodoma, Manyanya anasema wawekezaji wanatakiwa kuangalia fursa ya uwekezaji katika viwanda vya zao la zabibu kutokana na kutumika kutengeneza malighafi nyingi hapa nchini na nje ya nchi.

"Jambo ambalo litawapa faida kubwa kwenu na taifa kwa ujumla kwa kuwa zao la zabibu hutumika kutengeneza vitu mbalimbali kwa hiyo ni vema wawekezaji kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya zao hili," anasema Manyanya.

### KAMPUNI ZILIVYOJIPANGA

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Tanzania Distilleries (TDL), Devis Deogratius, anasema inatarajia kuingia mikataba ya moja kwa moja, ya kununua zabibu kutoka kwa wakulima wadogo, ikiwa ni dhamira ya kuendeleza kilimo cha zabibu, mkoani Dodoma.

Anasema kampuni kwa sasa inanunua takribani lita milioni 1.2 za mchuzi wa zabibu kwa mwaka kutoka kampuni mbili wakala na wazalishaji, zinazonunua zabibu za wakulima wa ndani.

Kwa mujibu wa meneja huyo, hadi sasa zimeshatumia Sh. bilioni 3.3 kwa mwaka na anadai kuwa imedhamiria kununua malighafi zinazozalishwa ndani ya nchi katika kipindi chote.

"Kwa sasa tunatumia malighafi na huduma za kufanikisha uzalishaji kwa asilimia 80, ambayo ni sawa na Sh. bilioni 46,"anaeleza.

Deogratius anasema, hatua iliyoko TDL imeshawekeza katika uundaji wa chapa za Kitanzania kwenye bidhaa za vinywaji kama vile anazitaja: Mvinyo wa Imagi, Valeur, Wines Dodoma, Dodoma Rose, Konyagi na Zanzi Cream liqueur, zenye ubora wa kimataifa, ikilenga mahitaji ya makundi mbalimbali sokoni.

Mkurugenzi huyo anasema, TDL inaamini kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya viwanda zinafanikiwa, sambamba na wakulima wadogo kuwezeshwa kuzalisha malighafi yanayohitajika viwandani.

### WAKULIMA WALONGA

Mkulima Samwel Mombo, anaeleza mtazamo wake kuwa viwanda vingi vya kuiongezea thamani zao hilo vikijengwa, vitasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji soko lake nchini na kumaliza tatizo la soko.

Mwingine, Emmanuel Temba, anasema kutokana na zabibu kukosa soko, walibuni wazo la mchuzi wa zao hilo, akilitolea ufafanuzi: "Zabibu inauzwa kama tunda bei yake ilikuwa imeshuka kwani inanunuliwa kwa Sh.400 kwa kilo kipindi cha masika na Sh.700 kwa kilo kipindi cha kiangazi na hali hii inasababisha kuendelea kuharibikia mashambani," anasema.

Anafafanua kuwa kutokana na uharibifu huo, waliamua kuanzisha Chama Cha Ushirika wa Wakulima Zabibu na Masoko Mpunguzi (UWAZAMAM) mwaka 2010, lengo ni kuwasaidia wakulima wa kijiji hicho kutafuta soko la zao la zabibu la ndani na nje.

Anasema kupitia chama hicho, walipata ufadhili wa kununua mashine ya kuchakata mchuzi wa zabibu ambao umekuwa na tija kwao na kuondokana na ukosefu wa soko.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tuwe makini na ahadi za wagombea






NA JOSEPH KULANGWA

KUNA kauli alipata kuitoa mtu maarufu duniani hivi sasa, Dk John Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba Watanzania si wajinga, hawadanganyiki. Alisema hivyo, alipokuwa akizungumzia tukio la uhalifu wa kiharamia kwa mtu mmoja nchini, ufafanuzi wake ukiacha viulizo.

Alikuwa akizungumzia sakata hilo na namna lilivyomalizika mikononi kwa wenye dhamana katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hakuingia kwa undani.

Bila shaka alikuwa na maana yake, kwamba Watanzania wa leo si rahisi kudanganyika, kwani wana uwezo wa kuona mambo, kuyachakata na kujua hili limekaaje, hili ni jema na hili si jema na kuchukua uamuzi.

Watanzania hao hivi sasa, wako kwenye mchakato wa uchaguzi, wanatafuta rais, wabunge na madiwani.

Kinachoendelea kabla ya Oktoba 28 ni kusikiliza hotuba zilizosheheni sera, ahadi na maneno matamu ya kutafuta ushawishi wa kupigiwa kura.

Watu wako kazini, watu hawalali, ni kampeni mpaka vyumbani, ni kampeni mpaka vitandani tunaambiwa. Watu wanatoa kauli zingine za kuvutia zikiwamo za kukera na za uongo pia, ili mradi kwenye mapambano kila mpiganaji huja na silaha yake na hachagui.

Hachagui silaha gani wala pa kupiga, ili mradi anahakikisha anashinda tu. Hivyo, wapo wagombea ambao bila shaka akili zao zinawatuma kuwa maneno na ahadi wanazotoa, ndizo zitakazowapa ushindi, wakisahau kuwa Watanzania hawadanganyiki. Wakisahau kuwa Watanzania si wajinga.

Anapanda jukwaani mgombea na kuahidi kulisha watu ubwabwa na kuku, samaki, nyama; mwingine anaibuka na ahadi ya kuhamishia bahari ya Hindi Dodoma, akitamba kuchimba mitaro ipite Morogoro hadi Dodoma. Sina uhakika kama ndiyo shida ya wakazi wa huko.

Huku, mwingine anakuja na ahadi ya kujenga daraja kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar. Anasema, haoni sababu ya watu kupanda boti zinazowatapisha, kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar na kurudi. Bahati mbaya hazungumzii ndege, kwa kuwa kajipanga kuhakikisha ajenda yake ya daraja inakubalika.

Kama haitoshi, anakuja mwingine, anasema akiingia Ikulu atahakikisha kila mkoa unanunuliwa ndege yake. Anataka watu wasafiri kwa ndege huyu, kana kwamba hakuna barabara wala reli. Hasemi nauli nazo atashusha na viwanja vya ndege atavijenga lini na vipi.

Jukwaa lingine mgombea mwingine anakuja na mengine, anahanikiza kwa sauti kubwa kabisa akiwa jimboni mwake, kwamba akiingia bungeni na kwa kuwa ana marafiki zake ni Marekani, basi watu wa jimboni mwake watabadilishana wa Marekani. Wa huku watakweda kule na wa kule watakuja huku.

Huyu anaamini kuwa kuwasaidia wananchi wake jimboni ni kuwapeleka Marekani. Pengine wapo wanaoamini hivyo, kwamba hayo ndiyo maisha na sijui wale wenzao wa Marekani wanaamini nini kuhusu kuja kubadilishana makazi na wenzao wa nchini!

Akimaliza huyo, anaibuka mwenzake naye anaahidi kujenga barabara za mabasi yaendayo haraka 'mwendokasi' jimboni mwake, ambamo hana hata barabara yenye urefu wa kilomita tatu zilizonyooka. Anajinasibu macho makavu mbele ya wapiga kura wake.

Anawaona wote waliofika mkutanoni mwake ni mabozi tu wasiojua lolote, wasiojua hata mchakato wa kujenga barabara za mwendokasi. Hawawaambii kuwa mradi huo unahusisha barabara maalumu, tena unajengwa kwa awamu nne jijini Dar es Salaam.

Hataki kujua kuwa ulianzia Kimara hadi Kivukoni, ukipinda kidogo hadi Morocco na Gerezani na sasa unaelekea Mbagala na hatimaye utaunganishwa kuelekea Pugu. Anaibuka na wa kwake jimboni na anautamka macho makavu, ili ashangiliwe. Anashangiliwa kweli. Kunabaki kiulizo cha kulikoni hao wanamshangilia.

Pengine wa ubwabwa anaweza kueleweka kuwa anachomaanisha si kulisha watu kila siku akiwa Ikulu, lakini angalau kuhakikisha watoto walioko shuleni wanapata mlo wa mchana kama ilivyokuwa zamani, ili wasisome na njaa. Lakini hawa wengine, hebu tuheshimiane kidogo jamani, sisi si wajinga.

Hawa wanaotudanganya Watanzania hawana tofauti na wanaotukana majukwaani, kwani kudanganya ni kumwona mwenzio mpumbavu au hawezi kutumia akili aliyopewa na Mungu wake. Watanzania tuendelee kuwa werevu, tuwasikilize, tuchambue na tuamue bila kujali itikadi wala mafiga. Alamsiki.

**Simu: (+255) 713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

# RC Ndikilo akagua uwekezaji mabilioni viwanda vya Kibaha

• Mitungi gesi 600,000 kila mwaka • Rekodi ya pekee Afrika Mashariki • Ajira 500,000, kodi Sh. bilioni 2.8



Mkurugenzi wa Kampuni ya Lake Oil, Frank Nyabundege, akimuelezea Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, namna mitungi ya gesi inavyotengenezwa. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

**Na Julieth Mkireri,** Kibaha

HADI sasa inajulikana, Pwani ni kati ya mikoa vinara nchini kwa kutekeleza kaulimbiu ya ujenzi wa viwanda. Ndani ya miaka mitano iliyopo, tayari kuna jumla ya viwanda 1,236 vimeshajengwa.

Mkuu wa Mkoa, Mhandisi Evarist Ndikilo, naye kwa nafasi yake amekuwa akiendelea kwa wakati wake kuhamasisha wawekezaji kufika mpakani kwake kujenga viwanda.

Hiyo inatokea huku kukiwapo miundombinu na mahitaji mengine muhimu yanayofanana kutimiza lengo hilo.

Aidha, amekuwa akifanya ziara za mara kwa mara kwenye Viwanda vilivyojengwa katika mkoa huo na vilivyoanza kufanya kazi kuwasikiliza wawekezaji changamoto wanazokabiliana nazo, ili zipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Ndikilo katika ziara hiyo, amekuwa akisisitiza taasisi wezeshi kuwaondolea vikwazo wawekezaji. Hapo inafanyika katika uwezeshaji wa kutoa vibali, vinavyoruhusu shughuli za uwekezaji.

Hivi karibuni, mkuu huyo wa mkoa katika ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya viwanda vitano vikubwa ndani ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha kukagua yake.

Tayari kuna ushuhuda wa maendeleo ya viwanda nchini,

> **Ukataji miti uliokithiri unakwenda kumalizika baada ya kiwanda hiki kuanzishwa, niwapongeze Lake Oil kwa kufanya uwakezaji huu ambao kwetu unamanufaa makubwa.**



kukiwapo uwekezaji mkubwa wa viwanda, kikiwamo cha kuunganisha magari kama malori na mengineyo, huku kukiwapo kiwanda kingine mahsusi kwa mabasi ya abiria, mitungi ya gesi na kwa dawa za binadamu.

Ndikilo anawaambia wawekezaji wa viwanda alivyotembelea, kwa kuwasihi kuzingatia haki na maslahi ya wafanyakazi wao.

Aidha, anawasisitiza kutumia benki zilizopo mkoani Pwani kuweka fedha na kukopa, huku akiahidi kushughulikia matatizo ya umeme, maji na barabara kwamba atazipatia ufumbuzi wa haraka.

Kwa mujibu wa Injinia Ndikilo, uwekezaji katika mkoa huo una hesabu ya viwanda 1236, unaogawanywa katika vikubwa 68, vya kati na vidogo 112 kila moja, huku vidogo kabisa jumla yao ni 888.

**RC ZIARANI**

Alifanya ziara katika kiwanda cha kuunganisha magari eneo la TAMCO Kibaha, kiwanda cha kuunganisha mabasi ya abiria na kingine kinachotengeneza dawa za binadamu, pia kiwanda cha mikate.

Kingine kinahusika na mitungi ya gesi, mabomba ya maji safi na nondo vilivyopo katika eneo la Visiga, Kibaha.

Akiwa katika kiwanda cha mitungi ya gesi, Mhandisi Ndikilo anaeleza, namna uwekezaji uliofanyika utakavyohitajiwa na matokeo chanya kwa Watanzania na aliwapongeza kwa kuwekeza katika mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa huyo anasema kiwanda cha mitungi kapokamilika kinatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha mitungi 600,000 kwa mwaka, ambayo ni sawa na asilimia 30 ya mitungi ya gesi inayoagizwa nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Mhandisi Ndikillo, ni bidhaa iyakayowafikia wananchi kirahisi na gharama nafuu, ukiwaondolea uharibifu wa mazingira na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa umma.

"Ukataji miti uliokithiri unakwenda kumalizika baada ya Kiwanda hiki kuanzishwa, niwapongeze Lake Oil kwa kufanya uwakezaji huu ambao kwetu unamanufaa makubwa, " anasema Mhandsi Ndikilo.

**WAZALISHAJI**

Mkurugenzi wa kampuni ya Lake Oil, Frank Nyabundege anaeleza kuwa, viwanda vyote vilivyopo Visiga kitakapokamilika na kufanya kazi, vitakuwa na uwezo wa kulipa kodi zaidi ya Sh. bilioni 2.8 kwa mwaka.

Akielezea uzalishaji wa mitungi ya gesi, anasema hadi uwekezaji wake kukamilika, utagharimu Sh. bilioni 18.8, kila mwezi kukizalishwa mitungi 50,000.

Frank anasema, mradi huo ni wa kwanza katika ukanda wa Afrika Masharikí na kupitia mradi huo, uchumi utakua kupitia matumizi ya nishati mbadala badala ya matumizi ya kuni na mkaa.

Mkurugenzi huyo anasema, uzalishaji mitungi ya gesi nchini, unatarajiwa kuleta chachu ya kushuka bei ya gesi inayowafanya Watanzania, wengi kumudu gharama za kununua gesi na kuachana na ukataji miti kwa ajili ya mkaa na kuni

Pia, kuna mradi mwingine wa kuzalisha nondo, uwekezaji nao hadi kukamilika unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 42.3 na Frank anaeleza kwa sasa inazalishwa tani 12 za nondo, kukiwapo matarajio ya kuzalishwa tani 25.

Mkurugenzi huyo anataja mradi mwingine wa kuzalisha mabomba ya maji safi, una uwekezaji thamani ya dola bilion 8.2 hadi kukamilika. Anasema, mradi huo wenye mitambo minne ya kuzalisha mabomba ya kusambaza maji safi, kila mmoja ina uwezo wa kuzalisha tani 1900 hadi 2000 kwa siku.

Frank anasema Viwanda hivyo vitatu vitakapokamilika katika awamu zote vitakuwa na uwezo wa kuzalisha ajira zaidi ya 500 za moja kwa moja.





# Mkakati wapunguza mauaji ya wazee

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa uwapo wa mkakati wa Taifa wa kutokomeza mauaji ya wazee nchini, umechangia kupunguza mauaji hayo hadi kufikia 74 kwa mwaka jana.

Akifungua kikao cha tathmini ya mkakati huo, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara kuu ya Maendeleo ya Jamii), Sayi Magese, alisema kwa mwaka 2014 kulikuwa na mauaji ya wazee 557, lakini hadi kufikia mwaka 2019, yamepungua na kuwa 74.

Alisema vifo hivyo vya wazee vilikuwa vinatokana na imani za kishirikiana ambapo wengi wao walikuwa wakiuawa wakati wa uchaguzi suala ambalo limekomeshwa kwa kiasi kikubwa.

"Inawezekana kutokomeza kabisa vifo hivyo na kipindi kama hiki cha uchaguzi ilikuwa hali mbaya sana, imani potofu tu, eti ukimuua unapata kura sio kweli, mkakati huu umesaidia sana kukomesha mambo ya mila na imani za kishirikina na kujengea uelewa wa jamii kutambua haki za wazee," alisema.

Awali, alisema sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonyesha kuwa idadi ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 60 Tanzania ni 2,507,568.

Aidha, alisema idadi hiyo ya wazee ni asilimia 5.6 ya Watanzania wote ambapo asilimia 80 ya wazee hao wanaishi vijijini.

"Wazee ni kundi muhimu katika jamii linalohitaji ulinzi na utetezi wa haki yao kwa kuwa katika umri huo, wengi wao wamekuwa hawathaminiwi baada ya kulitumikia Taifa kwa muda mrefu katika utumishi au katika jamii," alisema.

Hata hivyo, alisema kupitia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, serikali inajivunia mafanikio mbalimbali ikiwamo vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali vinatoa huduma za afya kwa wazee bila malipo.

Alieleza kuwa katika mpango wa utambuzi wa wazee katika Halmashauri hadi Machi 2020, Serikali imewatambua wazee 1,700,014 kati yao, wazee 933,790 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo.

Pia alisema Mabaraza ya Wazee 17,416 yameundwa nchi nzima na imesaidia kuwashirikisha wazee kwenye masuala mbalimbali yanayohusu ustawi na maendeleo yao.

Aliomba vyombo vya habari kuendelea kufichua uovu huo na kuelimisha jamii kuondokana na mila potofu zinazosababisha vitendo vya ukatili kwa watu wasio na hatia. "Vilevile, serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale wote watakaopatikana na hatia ya mauaji dhidi ya wazee," alisema.

Kwa upande wake, Meneja Programu, Haki za Wazee na ushirikiano wa wadau kutoka Shirika lisilo la serikali la Help Age International, Joseph Mbasha, alisema mkakati huo unalenga kukomesha mauaji ya wazee ili ifikapo mwaka 2023 Tanzania kuwe hakuna kifo cha mzee kwa imani potofu.

Alisema shirika hilo litaendelea na jukumu lake la kuhakikisha kunakuwapo na ustawi wa wazee kwa kushauri mabadiliko mbalimbali ya kisera na utendaji.

Naye Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema wizara hiyo ina wajibu wa kuhakikisha kunakuwapo na haki, ustawi na ulinzi wa wazee ambapo kutokana na miaka mitano iliyopita kukithiri kwa mauaji hayo, mwaka 2019 serikali ilizindua mkakati huo ili kutokomeza mauaji hayo ambayo ni aibu kwa Taifa.



Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas (kushoto), akikabidhi Bendera ya Taifa kwa maofisa, wakaguzi na askari katika ofisi za makao makuu ya jeshi hilo, jijini Dodoma jana, kabla ya kuanza safari ya kwenda kulinda amani nchini Sudan. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Wamachinga wapewa siri kupata mikopo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA ndogo (Machinga) wametakiwa kuboresha biashara zao, ili wapate mikopo itakayokuza mitaji yao na kuhimili ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi.

Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao alipowatembelea kwenye maeneo yao kukagua biashara zao.

Alisema kuwa wakiboresha biashara watajiimarisha kiuchumi na kuiinua mitaji badala ya kuendelea kufanya shughuli hizo kimazoea bila faida.

Aidha, aliwataka kuepukana na migogoro isiyo na tija ambayo mara nyingi imekuwa ikirudisha nyuma mafanikio yao kibiashara.

"Endeleeni kushirikiana na Halmashauri ya Jiji ambayo imekuwa ikiwapa maelekezo na kanuni za namna ya kufanya biashara kwa uhuru na ufanisi," alisema.

Alisema kuwa ili biashara istawi wafanye biashara kwa njia ya utulivu, amani pamoja na kuzitii mamlaka ambazo zipo kwa kufuata maelekezo wanayopewa badala ya kuwa na malumbano na mamlaka husika.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wilaya ya Dodoma, Baraka Mrisho, alipongeza Halmashauri ya Jiji kwa kuwawezesha kufanya biashara zao kwa uhuru unaozingatia kanuni na sheria za utunzaji wa mazingira.

"Awali tulikuwa tunazagaa maeneo mbalimbali bila mpangilio hali ambayo ilikuwa ikionyesha wazi kuwa ni waharibifu wa mazingira kutokana na kufanya biashara kwa kutangatanga na kusababisha msongamano ambao haukuwa wa lazima," alisema.

Aliomba Halmashauri ya Jiji kuhakikisha kuwa wamachinga wanaondolewa kwenye maeneo yasiyo rasmi hasa barabarani ili kuondoa misongamano ambayo inahatarisha maisha yao.

"Kuna wenzetu wengine wanafanya biashara zao pembezoni kabisa mwa barabara na wengine wamesogea kabisa barabarani, kitu ambacho kinahatarisha maisha yao, maana ikitokea na hatuombei dereva gari limemshinda sehemu ya kuegesha mfanyabiashara ameweka bidhaa zake, ataweka wapi si atajikuta anamwegeshea hapo hapo," alisema.

# Kongwa yajipanga kilimo cha korosho

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

WILAYA ya Kongwa ipo mbioni kuanza kutekeleza mpango wa kuhakikisha kila kaya inalima ekari moja ya zao la miche ya korosho bora ili kuongeza kipato na kurejesha hali ya uoto wa asili kwenye eneo hilo.

Akifungua mafunzo ya kilimo bora cha korosho yanayoendelea kutolewa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Naliendele kwa wakulima na maofisa ugani wa halmashauri wa wilaya hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Suleiman Serera, alisema hatua hiyo pia itapunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

"Mkakati wa Wilaya ya Kongwa ni kuhakikisha angalau kila kaya inakuwa na ekari moja ya zao la korosho bora sababu ni zao la kudumu la kibiashara lenye manufaa kiuchumi, lakini tunataka kuikijanisha Kongwa yetu kupitia mbegu bora za mikorosho kutoka TARI Naliendele," alisema Serera.

Alisema ili kukamilisha mpango huo tayari umeanza kutekelezwa kwa awamu itahitajika miche zaidi ya milioni mbili ili kuzifikia kaya zote 74,000 zilizopo ndani ya wilaya hiyo.

Serera alisema kilimo hicho katika wilaya hiyo kilianza rasmi msimu wa kilimo wa 2007/8 na mpaka sasa kuna jumla ya mikorosho mikubwa 75,591 na midogo 231,295, hivyo kuwa na jumla ya mikorosho 306,886 sawa na ekari 10,229.5.

"Naamini baada ya mafunzo haya maofisa ugani mtaendelea kutoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima kwenye maeneo yenu ili kuongeza tija na uzalishaji kwa ustawi wa wilaya yetu," alisema Serera.

Kwa upande wake, mratibu wa zao la korosho kitaifa kutoka TARI Naliendele, Dk. Geradina Mzena, alisema mafunzo hayo yana nadharia na vitendo yana lengo la kuongeza ujuzi kwa wakulima na maofisa ugani ili kuinua tija kwenye zao la korosho.

"Kwenye mafunzo haya pamoja na mambo mengine tutajikita katika kuangalia namna bora ya kuanzisha shamba jipya, 'Agronomia ya korosho' na namna bora ya kudhibiti wadudu na magonjwa ya zao hilo," alisema Mzena.





## ‘Wanawake msikubali kutumika kama madaraja’

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

WANAWAKE jijini Mbeya, wametakiwa kuepuka kutumiwa na wanasiasa hasa kipindi cha uchaguzi kama madaraja ya kuwavushia wanasiasa hao na badala yake wanatakiwa kuwashawishi wanasiasa kuwainua kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na mdau wa maendeleo mkoani hapa, Ndele Mwaselela, alipokuwa akizungumza na wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya na kwamba mara nyingi wanasiasa wanatumia wanawake kujinufaisha.

Alisema endapo kundi hilo muhimu kwa taifa litaendelea kukubali kutumiwa na wanasiasa, litaendelea kuwa maskini na kulalamikia hali ngumu ya maisha huku wanasiasa wakizidi kuchanua.

Mwaselela aliwaonya wanasiasa wanaowatumia wanawake hao kipindi cha kampeni za kisiasa na kuwaacha baada ya kupata wanachokitaka akiwataka kuacha tabia hiyo na badala yake watumie fedha zao kuwainua kiuchumi.

“Mkiendelea kutumika na wanasiasa, mtaendelea kuwa maskini wakati wenzenu wanazidi kuwa matajiri kwa kupitia migongo yenu, hivyo nawashauri mwendelee kufanya shughuli zenu kwa maslahi ya familia zenu, wakitaka waje wawasaidie mitaji,” alisema Mwaselela.

Aliwataka wanawake kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi kwa kuhakikisha wanawekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zenye ubora ili kuunga mkono juhudi za serikali za kufikia uchumi wa viwanda.

Aliwataka wanawake kuwa mstari wa mbele kuwekeza hata kama wana umri mkubwa kwa kwa madai kuwa kundi hilo ndilo lenye jukumu kubwa la kulea watoto.

Pia aliwataka wanawake hao kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha wanazopata ili kuendeleza biashara zao badala ya kuwa na matumizi makubwa kuliko kile wanachozalisha kuepuka kufilisika.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akiwa Kata ya Isyonje, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili wanawake ni mtaji unaosababisha washindwe kuanzisha biashara zao.

Pia, alisema mwitikio wao ni mdogo kujiunga kwenye vikundi ambavyo vitawasaidia kukopesheka na taasisi za kifedha pamoja na halmashauri.

# Wafugaji wapigwa marufuku mifugo hifadhini

Na Grace Mwakalinga,
MBARALI

KAMISHNA wa Uhifadhi Kanda ya Kusini, Pius Mzimbe, amepiga marufuku wafugaji kuingiza mifugo yao katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha pamoja na wananchi kutoingia kwenye hifadhi hiyo bila kibali kufanya shughuli za uvuvi na kwamba atakayebainika atafunguliwa kesi ya ujangili.

Mzimbe alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wanahabari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) kwa kushirikiana na Shirika la Watu wa Marekani (USAID), ambao walifika katika Ofisi ya Uhifadhi Kanda ya Kusini iliyoko Rujewa katika Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya.

Alisema miongoni mwa vikwazo vinavyoikabili Hifadhi ya Ruaha ni wafugaji kuingiza mifugo yao ndani ya hifadhi ikiwamo ng’ombe hali inayohatarisha afya za wanyamapori kutokana na magonjwa mbalimbali kama vile kimeta.

“Mara kwa mara tunatoa elimu na kuwakataza wafugaji kutoingiza mifugo ndani ya hifadhi kwa sababu wanaweza kuhatarisha afya za wanyamapori, mifugo yao na hata wao wenyewe, lakini bado ni wabishi hawasikii sasa tukiwabaini tutawafungulia kesi ya ujangili kwa sababu wanalengo la kuathiri urithi wetu,” alisema Mzimbe. Alisema mfugaji yeyote anayekamatwa ndani ya hifadhi akiwa na mifugo yake pamoja na wananchi wanaoingia hifadhini kuvua samaki wote hao tunawahesabia kama majangili hivyo hawaruhusiwi kuingia.

Aliwaomba wananchi wanaozunguka hifadhi zote za kusini kama vile, Ruaha, Kitulo na Katavi kuendelea kutunza na kuhifadhi wanyamapori na maliasili zote ili kukuza uchumi wa nchi.

Katika kuhakikisha mahusiano na ujirani mwema vinaendelea kuimarishwa kwa lengo la kutunza Hifadhi ya Ruaha, wananchi wa kata za Mawindi na Igava wameomba maofisa kuendelea kuzisaidia jamii hizo miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile ujenzi wa shule, maji na barabara.

Ofisa Mtendaji wa Mawindi, Hamo Gaudai, alisema licha ya TANAPA kusaidia ujenzi wa bwalo kwa Shule ya Sekondari Mawindi kwa zaidi ya asilimia 70, bado wanahitaji misaada mingine kama ujenzi wa barabara na madaraja ikiwa ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa wananchi.

Gaudai alisema kujengwa kwa miradi ya maendeleo kutachochea utunzaji na uhifadhi wa wanyamapori na maliasili kwa kuwa wananchi watanufaika na uwapo wake. Aliishauri TANAPA kubadili mfumo wao wa ujenzi kuacha kutumia kandarasi na badala yake iwe ‘Force Account’ (rasilimali za ndani) ili kubana matumizi na kujenga miradi hiyo kwa wakati.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mawindi, Mawazo, Ndanzi aliishuruku TANAPA kwa mradi huo wa bwalo ambalo ulisaidia shule hiyo kupata kibali cha kuanzisha kidato cha tano.

Alisema licha ya bwalo hilo kutokukamilika, lakini limefikia hatua nzuri kwa kuwa sasa wanalitumia kwa shughuli mbalimbali kama mikutano na mitihani pia aliwaomba TANAPA kuwasaidia mradi wa maji shuleni hapo.

Ndanzi alisema kwa sababu ya shule yake kuwa karibu na Hifadhi ya Ruaha baadhi ya vipindi, tembo hufika katika eneo hilo, lakini kwa sababu wanafunzi walipewa elimu ya kukabiliana au kuwakwepa hakuna aliyejeruhiwa wala kupoteza maisha



Kaimu Meneja Mwandamizi wa Kitengo cha Uhusiano wa Benki ya TPB, Chichi Banda (wapili kulia), akimkabidhi Ofisa Elimu wa Wilaya ya Musoma, Majidu Karugendo (kulia kwake), sehemu ya vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 9.5 vya ujenzi wa mabweni ya Shule ya Sekondari ya Kiriba, katika hafla iliyofanyika wilayani humo, mkoani Mara, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Imani potofu chanzo uharibifu mazingira

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

IMANI potofu miongoni mwa jamii za wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, zimetajwa kuwa ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira ikiwamo uchomaji ovyo wa misitu hali inayoathiri maisha ya viumbe hai.

Chifu wa Kabila la Wasafwa, Roketi Mwashinga aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu wajibu wa viongozi wa kimila wa kupambana na uharibifu wa mazingira.

Alisema imani potofu ambazo zinaaminisha watu kuwa baadhi ya uoto ni utajiri, umechangia kwa kiasi kikubwa kupoteza uoto wa asili na kusababisha jangwa au ukame. “Laiti machifu au wazee wa kimila wangekataa miti hovyo au kuharibu maliasili kizazi cha sasa kisingenufaika na uoto wowote wa asili na huenda kungekuwa ni jangwa ndio maana tumeamua kulivalia njuga ili kuhakikisha hakuna uharibifu wa mazingira,” alisema Mwashinga.

Aliongeza kuwa zipo baadhi ya imani kuwa kuchoma misitu kunasaidia kupata mazao mengi mashambani pamoja na kuwakamata kirahisi wanyama wa porini kwa ajili ya kitoweo na kwamba imani hizo zinaharibu ikolojia.

Alisema imani za aina hiyo ni za uongo na hazina faida kwa binadamu zaidi ya kuharibu mazingira ambayo ndiyo makazi ya viumbe hai mbalimbali wakiwamo wanyamapori, mimea, ndege pamoja na wadudu ambao wanapendezesha mazingira.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba, alisema elimu ya utunzaji wa mazingira ambayo inatolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imesaidia kupunguza tatizo la uharibifu wa mazingira wilayani humo.

Alisema kwa sasa wamefanikiwa kudhibiti vitendo vya uchomaji misitu ovyo na wananchi wameanza kuelewa madhara ya matukio hayo na wanahamasishana wao wenyewe kulinda misitu.

Aliongeza kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la upandaji miti jambo ambalo limesaidia utunzaji wa kimazingira na wanategemea elimu hiyo itasaidia kuifanya wilaya hiyo kuwa kinara utunzaji mazingira nchini.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya hiyo walisema kutokana na elimu waliyoipata ya utunzaji wa mazingira, watahakikisha wanayalinda hasa misitu ili waondokane na matatizo yanayowakabili ikiwamo ukosefu wa maji.

Mmoja wa wananchi hao, Ambokile Samwel, alisema tangu walipoanza kupewa elimu wamekuwa na mwamko wa kulinda mazingira ikiwamo vyanzo vya maji kwa kupanda miti na kuzuia mifugo kuingia kwenye maeneo hayo pamoja na kuhakikisha kila mmoja anashiriki kuzuia moto.



# Mwinyi aibua staili mpya ya kampeni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, amebadili staili ya kampeni zake kwa kukutana na makundi mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara wadogo.

Staili hiyo ya kampeni aliianza mapema wiki hii, huku kwa mara ya kwanza akikutana na wajane na watu wa makundi maalum na kusikiliza kero zao, huku akiahidi iwapo atachaguliwa atazifanyia kazi ikiwamo kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

Juzi, akisikiliza kero za wafanyabiashara wa soko la Kijangwani, wafanyabiashara wa soko hilo walisema janga la corona limesababisha mitaji yao kufa na biashara kuwa ngumu.

Walisema awali walikuwa wakiuza bidhaa zao katika Soko la Darajani Mjini Zanzibar, lakini lilipoingia janga la hilo waliondolewa na kuwekwa Kijangwani.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Halima Ali, alisema corona imeua mitaji yao, hivyo kumwomba mgombea huyo kutunisha mfuko wao ili kuendeleza biashara zao.

Alisema eneo hilo la Kijangwani si wateja wengi wanaofika hapo tofauti na walipokuwa Darajani ambako biashara ilikuwa nzuri kutokana na eneo hilo kufikiwa na watu mbalimbali wakiwamo watalii.

Naye mfanyabiashara Kheir Ameir Kheir, alimwomba Dk. Mwinyi endapo atashinda na kuwa Rais wa Zanzibar, kuboresha miundombinu katika soko hilo ili kuondokana na changamoto zinazowakabili.

Alimtaka pia mgombea huyo kuendelea na ziara zake hizo hata baada ya kupata urais kwa sababu wananchi wana kero nyingi, lakini wanashindwa kumfikia Rais kueleza changamoto zao.

Baada ya kusikiliza kero hizo, Dk. Mwinyi alisema endapo wananchi wa Zanzibar watamchagua atahakikisha kila manispaa na halmashauri zinajengewa masoko ya kisasa kwa wafanyabiashara wadogo katika mji wa Zanzibar.

Alisema mpango huo unaendana na utekelezaji wa ilani ya CCM ya 2020 inayotilia mkazo kuimarisha uchumi wa wafanyabiashara wadogo na fursa muhimu za kuongeza pato la serikali na usimamizi wa maeneo hayo.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na wafanyabiashara wa eneo la Sateni Mjini Zanzibar jana, kwa lengo la kusikiliza kero zao na kuomba kura. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wakemea vitendo vya uvunjivu wa amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI mbalimbali wa serikali na dini visiwani Zanzibar, wamekemea kitendo cha kushambuliwa kwa mapanga watu watatu wanaosadikiwa kuwa makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) hivi karibuni walipokuwa msikitini huko kisiwani Pemba.

Wakizungumza kwa nyakati fotauti, viongozi hao walisema kitendo hicho kinapaswa kukemewa huku serikali ikisisitiza kuwa haitakuwa na mswalie mtume na watu wanaojihusisha na vitendo vya uvunjifu wa amani kuelekea uchaguzi.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema juzi kuwa serikali haitamvumilia mtu au kikundi chochote kitakachojihusisha na vitendo vya aina hiyo hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi na baada ya kutangazwa matokeo.

Alisema hayo wakati akimfariji na kumpa pole msanii mkongwe wa muziki wa taarabu Zanzibar, Khamis Nyange Makame, maarufu kama Profesa Gogo, aliyelazwa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja akipatiwa huduma za matibabu baada ya kushambuliwa kwa mapanga alfajiri ya Jumatatu.

Profesa Gogo na wenzake wawili walishambuliwa kwa mapanga wakiwa kwenye Ibada ya Sala ya Alfajiri, kijijini kwao Kangagani Wete, kisiwani Pemba na kupelekwa hospitalini kwa huduma ya kwanza na baadaye kusafirishwa katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja. Alisema inasikitisha kuona kwamba jamii nzima ikiongozwa na viongozi wa dini, wamekuwa katika ibada mbalimbali za kuliombea taifa kuendelea kuwa na amani wakati wote, lakini bado wako baadhi ya watu wanadiriki kuichezea amani hiyo.

Hata hivyo, Balozi Iddi aliwatoa hofu wananchi kwamba uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika mwezi ujao, utafanyika kwa amani na kila mwenye haki ya kuchagua na kuchaguliwa atapata fursa ya kushiriki kwa maendeleo na ustawi wa taifa.

Katika hatua nyingine, CCM Zanzibar, imesema viashiria vya kupigwa watu katika nyumba ya ibada kisiwani Pemba visiwatikise na badala yake kufanya uamuzi sahihi wakati wa uchaguzi.

Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Itikadi na Uenezi Zanzibar, Catherine Peter Nao, aliyasema hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui kutokana na kujeruhiwa kwa watu watatu kisiwani Pemba.

Alisema umefika wakati kwa wananchi kuwakataa wale wote wanaochochea vurugu katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi.

Pia alisema watu wanaofanya matukio ya kihalifu wana lengo la kuwatia hofu wananchi kutoshiriki katika mikutano ya kampeni na uchaguzi mkuu kwa kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua.

Pia Kamati ya Amani Zanzibar imeelezea kusitikishwa na tukio hilo lililotokea kisiwani Pemba ambalo linaashiria uvunjifu wa amani.

Akizungumza kwa niaba ya Mufti wa Zanzibar, Mkuu wa Fatwa na Utafiti, Shekh Thabit Nomal Jongo, alisema kitendo cha kuanza kumwagika damu ndani ya nyumba ya ibada ni kitendo cha kinyama.

Alisema ni vyema kwa wananchi kwamba tofauti zao za kisiasa zisiwafanye kufanya unyama ambao utapelekea kuichafua amani ya nchi.

Naye Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, Augustine Shao, alisema amani ni kila kitu katika taifa la Tanzania ili wananchi wafanye shughuli zao za kujipatia kipato bila ya bughuza.

Askofu huyo aliwataka waandishi wa habari kuendelea kutumia kalamu zao kuelimisha jamii juu ya suala la kulinda amani ya nchi wakati wote.

# Polisi yawaonya madereva Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadh Juma Haji, amewataka wananchi na wafuasi wa vyama vya siasa kufuata sheria za barabarani wanapokwenda na kurudi katika mikutano ya kampeni za kisiasa inayoendelea kila mahali.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi habari ofisini kwake, Mwembe Madema.

Kamanda Awadh alisema katika kipindi cha kampeni za kuelekea uchaguzi mkuu, kumeibuka tabia kwa baadhi ya waendesha vyombo vya moto kuvunja sheria za usalama barabarani kwa makusudi.

Alisema hali hiyo inahatarisha usalama wa maisha kwa watumiaji wa vyombo hivyo na watumiaji wengine wa barabara hizo.

Miongoni mwa makosa hayo, alisema ni pamoja na kupakia abiria kwa njia ya hatari na kujaza abiria kupitia uwezo wa gari.

Alisema makosa mengine ya uvunjaji wa sheria za barabarani ni pamoja na kuendesha kwa mwendo wa kasi na hatari, abiria kucheza muziki wakiwa ndani ya gari likiwa katika mwendokasi.

"Pia vyombo vya maringi mawili hubeba zaidi ya watu wawili, huendesha kwa mwendo wa mbwembwe zinazohatarisha usalama wa watumiaji wengine wa barabara," alisema kamanda huyo.

Aidha, alieleza kuwa pia kuibuka tabia ya kufunika namba za usajili za magari na vyombo vya maringi mawili kwa kuweka stika na bendera za vyama zinazoficha namba za usajili jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema vitendo hivyo vinaweza kutoa mwanya kwa wahalifu kufanya hivyo ili kuficha uhalisia wa namba za vyombo vyao kwa lengo la kufanya wasikamatwe kirahisi pindi watakapofanya uhalifu na kusababisha ajali za barabarani na kukimbia.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**

### VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa eneo la Mkundi/Banana mtaa wa bwawani -Morogoro. Ina vyumba vinne self container, sebule, dining room na choo cha nje ndani ya fensi. Wasiliana na simu 0713-435172/0713-440436.

### VIWANJA/MASHAMBA

**ENEO LINAUZWA,** Eneo linauzwa Makongo juu Dar-es-salaam karibu na Petrol Station mwisho wa lami Lina Nyumba nne za kuishi, umeme, maji ya kisima na dawasco ipo ndani ya fensi. Wasiliana na simu: 0753-029141/0779-999041.

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

### KUPOTEA KWA CHETI



**FATNA STEVEN KADEGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo chenye namba **IRDP/CRP/10/1274** kilichotolewa na Chuo cha Mipango Dodoma mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CHA/B.I/20/WDMA/180.**

115915602

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAWENI LIMESTONE LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 528 CGK.** CHASSIS NAMBA **SR400154401.** ENGINE NAMBA **3S5098594.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **DAR/MAG/RB/688589/2020.**

115915702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;288/2020**

**Ombi la LAMECK JULIUS MWAKALINGA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NAZIEL HANAEL MJEMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 27/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **23/09/2020.**

Tarehe 23/09/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115915502

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe **25/09/2020** kampuni ya chico **(China Henan Internation Cooperation Group Co. Ltd** itapitisha gari lenye namba za usajiri **T507 BKM / T509 BKM,** yenye **escort no T643 CVZ** likiwa halijabeba kitu kutoka **DODOMA** kuelekea **TABORA** kupitia **ITIGI ,**

2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - mita 3.00m**
   **Kimo - mita 4.5m**

3. Njia itakayo tumika ni **DODOMA hadi TABORA kupitia ITIGI** Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

*Tunaomba radhi kwa usumbufu*

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe **26/09/2020 kampuni ya chico (China Henan Internation Cooperation Group Co.Ltd)** itasafirisha mzigo **D45 DRILLER MACHINE** wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TABORA kuelekea DODOMA kupitia ITIGI** , gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM / T509 BKM** ,yenye **escort no T643 CVZ**

2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - mita 3.00m**
   **Kimo - mita 4.5m**

3. Njia itakayo tumika ni **TABORA hadi DODOMA** kupitia **ITIGI** Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

*Tunaomba radhi kwa usumbufu*

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONAVENTURE CHARLES SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **FORESTER SUBARU** yenye namba za usajili **T.950 CHY.** Chassis namba **SG5007939.** Engine namba **EJ203022217.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taaarifa ya polisi **MBE/CHU/RB/499411/2020**

115915202

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT** COMPANY LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 706 BQG (KINGLION KL 150-8).** Chassis namba **L7GPCJIY9G1079785.** Engine namba **KL154FMI-2G5079785.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/KIJ/RB/680737/2020.**

115915102

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**R.C TRUCKING (T) LIMITED** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 980 AYU. ENGINE NO 5714707. CHASSES **S NO 4377213.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/684022/2020.**

115914902

## Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

### TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki wa Kampuni ya **WAAD KHAYR COMPANY LIMITED** namba ya usajili **141164740** ya tarehe **09/01/2020** wanapenda kuutangazia umma kuwa Kampuni yao imefilisika na hivyo kuamua kuifunga kwa mujibu wa sheria ya Makampuni Brela.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;287/2020**

**Ombi la IFRAH HASSAN OMARY.,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NURIA MOHAMED NOOR MOHAMED.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/09/2020.

Tarehe ..../20....
Sahihi ya Hakimu

115914402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**Anuari ya simu "ARDHI"** **Baraza la Ardhi na Nyumba**
**Telefax 23244** **S.L.P 3194,**
**Telex2271** **ARUSHA**
**Unapojibu tafadhali taja:**

**MAOMBI NA 362 MWAKA 2019**

**HIYASINTA BILA................................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH BILA**
**MWAVITA WAZIRI...............................................MDAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: MWAVITA WAZIRI.....................POPOTE**

**HIYASINTA WOLTA MSABILA,** Amefungua maombi ya utekelezaji hukumu mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba na Wilaya ya Arusha. Shauri husika limepangwa kutajwa mbele ya Mh. G. Kagaruki,Mwenyekiti tarehe 15/10/2020 saa tatu kamili asubuhi. Hivyo basi,unatakiwa kufika kwenye baraza tarehe na muda uliotajwa kwa ajili ya kujibu maombi hayo. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba Arusha. Endapo hutatekeleza haya,shauri hili litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa dhidi yako. Ofisi za Baraza zipo katika Jengo la Mkuu wa Wilaya Arusha.
**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 09 mwezi Tisa mwaka 2020.

G. Kagaruki
MWENYEKITI

115916002

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Mradi elimu ya jinsia wapingwa Zambia

**LUSAKA,** Zambia

MRADI wa elimu ya jinsia nchini Zambia ambao unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), umekataliwa na Waziri wa Masuala ya Dini, Godfridah Sumaili, nchini humo.

Sumaili alinukuliwa na vyombo vya habari nchini humo akisema mradi huo unahamasisha kujitambua kijinsia, mapenzi ya jinsia moja na haki za kigeni za afya ya uzazi.

"Zambia ni taifa linalofuata mlengo wa kikristo na hivyo tunapaswa kulinda maadili yetu ya kikristo," alisema.

Kanisa la kiinjili la kikristo pia lilipinga mradi huo, lakini kulikuwa na mvutano mkubwa kutoka katika makundi mbalimbali ambayo yalionyesha kuunga mkono.

Tovuti ya Umoja wa Mataifa ilisema mradi huo unajumuisha taarifa sahihi kuhusu maendeleo ya binadamu na afya ya uzazi, pamoja na taarifa za mpango wa uzazi na magonjwa yanayoambukiza kupitia ngono. **BBC**

## Upinzani wailaumu serikali kupinga ukomo wa katiba

**BANJUL,** Gambia

KIONGOZI wa upinzani nchini Gambia ameilaumu serikali kwa kukataa rasimu ya katiba inayoainisha ukomo wa urais.

Bunge la nchini humo lilikataa katiba hiyo Jumanne.

Kipengele kinachomzuia Rais Adama Barrow, kuweka muda wa ukomo wa utawala kwa mihula mingine miwili kinaonekana kuwa hatua kubwa ya mshikamano.

Kiongozi wa chama cha United Democratic Party (UDP), Ousainou Darboe, alisema mapendekezo hayo yalikuwa siyo dalili nzuri ya demokrasia.

Uchaguzi mkuu ujao umepangwa kufanyika mwakani.

Darboe ameapa kuitambulisha tena rasimu hiyo ya katiba kama upande wa upinzani ukishinda uchaguzi.

Rais Barrow aliingia madarakani mwaka 2016, baada ya kumalizika kwa utawala wa kimabavu wa Yahya Jammeh uliodumu kwa miaka 22. **BBC**

# Trump hayuko tayari kuachia madaraka

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amekataa kujitolea kupokezana madaraka kwa amani katika uchaguzi mkuu wa Novemba.

Akizungumza na waandishi wa habari Ikulu ya White House, Rais Trump alisema wataona kitakachofanyika wanajua hilo.

Alisema anaamini matokeo ya uchaguzi huenda yakaamuliwa katika mahakama ya juu zaidi, huku akisisitiza mashaka yake kuhusu upigaji kura kwa njia ya posta.

Majimbo zaidi yanatoa wito wa upigaji kura kwa njia ya posta, yakisisitiza umuhimu wa wapiga kura kuwa salama dhidi ya maambukizi ya corona.

Rais Trump kama atajitolea kukubali matokeo ya uchaguzi akishinda, kupoteza au kutoka sare dhidi ya mgombea wa Democrat Joe Biden.

"Napinga vikali upigaji kura kwa njia ya posta, na upigaji kura wa namna hii ni majanga," alisema.

Alipoulizwa kuhusu maandamano ya watu, Rais Trump alisema, "Futilieni mbali uchaguzi, na kutakuwa na amani hakutakuwa na suala la kupokezana madaraka, kwa kweli, kutakuwa na mwendelezo."

**Nadhani ni vyema tukienda kwa uchaguzi, kwa sababu nafikiria hii ni njama inayochezwa na Democrats, na njama hiyo itafikishwa mbele ya Mahakama ya juu zaidi ya Marekani.**

Mwaka 2016, Rais Trump pia alikataa kujitolea kukubali matokeo ya uchaguzi katika kinyang'anyiro kati yake na mgombea wa Democratic, Hillary Clinton, hatua ambayo alitaja kama shambulio dhidi ya demokrasia ya Marekani.

Hatimaye alitangazwa kuwa mshindi, licha ya kuwa hakupata kura za wengi ambazo pia bado anatilia shaka.

Mwezi uliopita, Clinton alimuomba Biden mara hii asikubali kushindwa katika mazingira yoyote katika mbio za mwisho usiku wa uchaguzi.

Alielezea hali ambapo Warepublican wangelijaribu kuwatumia ujumbe wapigaji kura ambao hawajapiga kura na kutumia kundi la mawakili kupinga matokeo ya uchaguzi. Wahafidhina wamemlaumu Biden kwa kuchochea vurugu katika uchaguzi aliposema mwezi Augosti kuwa, "Kuna mtu anaamini hakutakuwa na vurugu nchini Marekani ikiwa Donald Trump atachaguliwa."

Jumatano, Rais wa Marekani alitetea uamuzi wake wa kumtafuta Jaji wa Mahakama ya Juu zaidi kabla ya uchaguzi kujaza nafasi iliyoachwa wazi na marehemu Ruth Ginsburg, akisema kuwa anatarajia matokeo ya uchaguzi yakifikishwa mbele ya mahakama hiyo.

"Nafikiria uchaguzi utaishia Mahakama ya Juu zaidi, nadhani ni muhimu tuwe na majaji tisa," Rais Trump alisema.

"Nadhani ni vyema tukienda kwa uchaguzi, kwa sababu nafikiria hii ni njama inayochezwa na Democrats, na njama hiyo itafikishwa mbele ya Mahakama ya juu zaidi ya Marekani."

Trump alikuwa anaashiria kwa mara nyingine madai yake yaliozua utata kwamba kura inayopigwa kupitia mfumo wa posta inaweza kuibiwa.

Rais alisema atamteua jaji wa kike kuongoza mahakama hiyo Jumamosi ambaye atachukua nafasi ya Jaji Ginsburg, aliyefariki Ijumaa iliyopita. **BBC**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas (54), akivaa barakoa kujikinga na virusi vya corona. Maas amejiweka karantini baada ya mmoja wa walinzi wake kupata maambukizi. **PICHA: MTANDAO**

# Mjadala upimaji corona kabla ya ndoa waibuka

**KIGALI,** Rwanda

SUALA la kuwataka wanandoa na wageni wao kupima corona kwa gharama zao za dola za kimarekani 50 kwa kila mtu ili kuwaruhusu kufanya sherehe za baada ya kufunga ndoa, linaendelea kuzua mjadala mkali nchini Rwanda.

Wakati huu wa corona, ni wageni 30 tu wanaoruhusiwa kuhudhuria sherehe za harusi kulingana na hatua iliyowekwa na serikali ili kuzuia kuenea kwa virusi vya ugonjwa huo nchini humo.

Gharama hizo zinafanya baadhi kuamua kufanya hafla ya kanisani tu pasipo kusherehekea harusi huku wengine wakiziahirisha.

Manzi Jules na mke wake, Solange ambao wamefunga pingu za maisha katika kanisa la Mtakatifu Bosco mjini Kigali, hawakuwa na sherehe zozote baada ya ibada ya ndoa.

Na siyo kwamba sherehe zimekatazwa, la hasha ni kuambatana na maagizo yaliyopo ya kuzuia maambukizi ya corona.

Agizo la serikali linahitaji kwamba kufanya sherehe yoyote ya harusi, wanandoa na wageni wao lazima wawe na uthibitisho kuwa walipima corona na hawana virusi hivyo.

"Tuliamua kuja kanisani kupata baraka za Mwenyezi Mungu tu, isingewezekana kupima waalikwa wote 30, ingenigharimu franga milioni moja na nusu (dola 1500) tutafanya sherehe muda utakaporuhusu," Manzi Jules alisema. **BBC**




# ARTETA AFUNGUKA HATIMA YA OZIL

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amebainisha itakuwa ni vigumu kwa Mesut Ozil kupata nafasi ya kupenya kwenye kikosi cha kwanza cha washikabunduki hao.

Mkataba wa Ozil unamalizika mwishoni mwa msimu huu na nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, majaliwa yake hayajulikani baada ya kukataa kukatwa mshahara wakati wa mlipuko wa virusi vya corona.

Awali kikosi cha Arsenal kilikataa kukatwa asilimia 12.5 ya mishahara kwa kipindi cha miezi 12, baada ya Arteta kuripotiwa kuingilia kati.

Lakini, Ozil alikataa kukatwa mshahara wake na hivyo kumfanya kuingia kwenye mvutano huku akikataa kuondoka.

Mchezaji huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ujerumani hajaichezea timu hiyo, tangu kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu England, kwani kwa mara ya mwisho aliichezea Machi 7, mwaka huu dhidi ya West Ham na hakuwapo kwenye mchezo wa ushindi wa mabao 2-0 wa Kombe la EFL raundi ya nne dhidi ya Leicester City, Jumatano.

Arteta alikumbana na maswali kutoka kwa waandishi baada ya mchezo huo, wakihoji nafasi ya Ozil kwenye kikosi hicho na akabainisha atakuwa na wakati mgumu kuingia kwenye kikosi cha kwanza.

"Timu jinsi ilivyo unaweza kuona inaimarika," alisema akiwaambia waandishi wa habari. Tunataka kucheza kwa ubora zaidi na kumaliza kila mchezo kwa ushindi.




## *Barca yamuuza Suarez Atletico*

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imemuuza rasmi straika wake, Luis Suarez kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Atletico Madrid kwa euro milioni sita, Blaugrana hao wamethibitisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alikuwa kwenye mwaka wake wa mwisho pale Camp Nou na alikuwa kwenye wakati mgumu tangu msimu uliopita.

Jumatano, Atletico ilikubali kumpeleka Alvaro Morata kwenda Juventus kucheza kwa mkopo na hivyo kuacha nafasi kwa Suarez kuongezwa kwenye kikosi hicho cha Diego Simeone.

Mechi 22 alizoanza kwenye Ligi na mabao 16 aliyofunga Suarez msimu wa 2019-20, ilikuwa ni idadi ndogo sana tangu asajiliwe na klabu hiyo kutoka Liverpool mwaka 2014.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay alishinda mataji manne ya Ligi Kuu Hispania na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwa ni kati ya mataji 13 aliyoshinda akiwa hapo Barca kwa misimu sita.

## Lampard atarajia makubwa kwa Havertz

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Frank Lampard, anatarajia makubwa zaidi kutoka kwa Kai Havertz baada ya kufunga mabao matatu dhidi ya Barnsley.

Havertz hakuwa kwenye kiwango cha kuvutia katika mechi zake mbili za mwanzo za Ligi Kuu England, lakini 'hat-trick' yake ya Jumatano kwenye ushindi wa 6-0 katika Kombe la EFL, alionekana kwenye ubora wake katika mchezo uliopigwa pale dimba la Stamford Bridge.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani, pia alihusika na bao jingine katika mchezo huo kwa kikosi hicho cha Lampard.

Na sasa Lampard amepaza sauti yake na kusema kwamba, kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

"Nimefurahishwa na Kai na kila kitu alichokifanya usiku huu, kwani hicho ndio nilichokuwa nakitaka kutoka kwake," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Ulikuwa wakati mzuri zaidi kwake, naamini kuna mengi mazuri zaidi yanakuja katika mechi nyingine."

Tammy Abraham alicheza mbele ya Havertz na alifunga bao la ufunguzi, huku Ross Barkley na Olivier Giroud kila mmoja akifunga moja."



# De Boer kocha mpya Uholanzi

**AMSTERDAM,** Uholanzi

FRANK de Boer ameteuliwa kuwa kocha mpya wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Shirikisho la Soka la Uholanzi (KNVB), limethibitisha.

Ronald Koeman aliondoka katika nafasi hiyo na kwenda kuchukua mikoba ya kuinoa Barcelona baada ya kufukuzwa kwa Quique Setien.

De Boer, ambaye aliichezea Uholanzi mechi 112 na kucheza michuano miwili ya Kombe la Dunia, amesaini mkataba wa miaka miwili na atakuwa na kazi ya kuipeleka timu hiyo kwenye fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka 2022.

Mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 50, alianza vizuri kazi yake ya ukocha, wakati alipoiongoza Ajax kushinda mara nne mfululizo taji la Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie kati ya mwaka 2011 na 2014.

Hata hivyo, uteuzi huo umekuwa kama wa kushangaza kwa kiasi fulani, baada ya kuwa na rekodi mbaya tangu alipoondoka katika klabu hiyo ya Amsterdam.

Alikaa siku 85 kama kocha wa Inter Milan kabla ya kutimuliwa na baadaye alidumu kwa wiki 10 tu akiwa kocha wa Crystal Palace.






# PSG KUMKOSA DI MARIA MECHI NNE

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain itakuwa bila ya Angel Di Maria kwa mechi nne baada ya mchezaji huyo kufungiwa kwa kosa la kumtemea mate mlinzi wa Marseille, Alvaro.

Di Maria amekumbana na adhabu hiyo baada ya kuhusika kwenye vurugu za mchezo uliopigwa Septemba 13, mwaka huu.

Neymar, ambaye alimshutumu Alvaro kwa ubaguzi wa rangi, kitu ambacho mchezaji huyo alikikana, huku Leandro Paredes na Layvin Kurzawa wote wakiwa wametolewa kwa kadi nyekundu hapo PSG, pamoja na Dario Benedetto na Jordan Amavi kwa upande wa Marseille.

Huku Neymar ameanza kutumikia adhabu yake, Di Maria atakosa mechi nne kwa mabingwa hao wa Ligue 1.

Hata hivyo, kocha Thomas Tuchel ataweza kumtumia raia huyo wa Argentina katika mchezo wa Jumapili hii dhidi ya Reims, kwani adhabu yake itaanza Septemba 29.

Di Maria atakosa mechi za PSG kwenye Ligi Kuu dhidi ya Angers, Nimes, Dijon na Nantes.

# *Atletico wagoma kumuuza Gimenez*

**MADRID,** Hispania

ATLETICO Madrid imekataa dau la pauni milioni 78 kutoka kwa Manchester City, ili kumuuza Jose Gimenez, rais wa klabu hiyo ya LaLiga, Enrique Cerezo amethibitisha.

Gimenez mwenye umri wa miaka 25, amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda City na gazeti la AS liliripoti mwezi huu kwamba, Atletico imeikataa ofa hiyo kutoka kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Cerezo alithibitisha kwamba miamba hao wa LaLiga walipata ofa kutoka kwa City, lakini wao wameamua kumbakiza mlinzi huyo hapo kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

"Tulipokea ofa kwa ajili yake," alisema akiiambia El Transistor.

"Lakini Gimenez ni mchezaji ambaye ni muhimu sana kwetu na kwa timu yetu, hivyo tumeamua abaki kwenye timu."

Baada ya kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa LaLiga msimu uliopita, Atletico ambao wamekubali kumsajili nyota wa Barcelona, Luis Suarez, wataanza kampeni ya msimu huu mpya wa ligi kwa kucheza na Granada nyumbani, Jumapili hii.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MENDY MAMBO MAZURI CHELSEA

●●● Golikipa huyo anatarajiwa kuwa chaguo la kwanza la Lampard ambaye amejipanga...

**LONDON,** England

CHELSEA imefanikiwa kumsajili golikipa, Edouard Mendy (28), kwa mkataba wa miaka mitano.

**Nyota huyo wa kimataifa kutoka Senegal ameichezea klabu ya Rennes mechi 25 za Ligue 1 tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2019 akitokea Reims.**

Alikamilisha vipimo vya afya Jumanne wiki hii na Kocha Frank Lampard alisema anataka kuongeza ushindani kwa golikipa aliyeweka rekodi ya usajili ya klabu hiyo ya pauni milioni 71, Kepa Arrizabalaga.

"Nimefurahi sana kujiunga na Chelsea," alisema Mendy.

"Ilikuwa ni ndoto yangu kwa kufanikiwa kuwa sehemu ya kikosi hichi. Nina hamu kubwa ya kukutana na wachezaji wenzangu pamoja na kuanza kuitumikia klabu hii," Mendy alisema.

Mendy anakuwa mchezaji wa saba kutua Stamford Bridge na amejiunga The Blues kwa dau la pauni milioni 22, na anatarajiwa kukiongezea nguvu kikosi cha Frank Lampard.

Mendy sasa anatajwa kuwa golikipa chaguo la kwanza la Chelsea kutokana na Lampard 'kuvurugwa' na makosa ya mara kwa mara ya Arrizabalaga.

Chelsea imeruhusu nyavu zake kutikiswa mara 54 katika mechi 38 za Ligi Kuu England msimu uliopita na Lampard anataka Mendy asaidie kumaliza rekodi hiyo mbaya iliyowekwa na timu hiyo.

Ujio wake unaifanya Chelsea iwe imetumia kiasi kisichopungua pauni milioni 250, huku nyota wengine waliosajiliwa ni pamoja na Hakim Ziyech, Timo Werner, Ben Chilwell, Malang Sarr, Thiago Silva na Kai Havertz.

Baada ya kufanikisha usajili huo wa Mendy, Mkurugenzi wa Chelsea, Marina Granovskaia, alisema: "Hivi karibuni Petr Cech na Idara ya Ufundi itamtangaza Edouard kama ndiye golikipa anayetufaa na amekamilisha kikosi tulichokuwa tunakihitaji, amebaki mchezaji mmoja tu ambaye tunamhitaji kwenye timu yetu.

## ZISIKUPITE

### TELLES AITAKA UNITED

BEKI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Brazil, Alex Telles (27), anataka kuondoka Porto na kujiunga na Manchester United, huku akijaribu kupunguza dau lililowekwa la pauni milioni 36.3, ili kufanikisha mchakato huo. ***(Telegraph - subscription required)***

### MANE KUMVUTA KOULIBALY

LIVERPOOL inataka kumtumia mshambuliaji wake, Sadio Mane kufanikisha usajili wa Msenegali mwenzake, Kalidou Koulibaly kujiunga na timu hiyo akitokea Napoli, licha ya Manchester City na Paris St-Germain kutajwa kumwania beki huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Le Parisien, via Sun)***

### RUDIGER ANUKIA PSG

PSG imeweka wazi inataka saini ya beki wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger (27), kwa mkataba wa muda mrefu. ***(Mail)***

### SMALLING AIVUTIA ROMA

ROMA inataka kupeleka ofa ya pili kwa Manchester United ili kumnasa beki wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Chris Smalling (30), ambaye aliitumikia kwa mkopo klabu hiyo ya Serie A msimu uliopita. ***(Guardian)***

### TORREIRA ANUKIA ATLETICO

MABOSI wa Atletico Madrid wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Uruguay, Lucas Torreira, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### UNITED, WEST VITANI

WEST Ham iko tayari kupambana na Manchester United kuwania saini ya beki wa kati wa Swansea City na Timu ya Taifa ya Wales, Joe Rodon, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Guardian)***

### VILLA WAMTAKA BARKLEY

ASTON Villa inajiandaa kuwasajili kwa mkopo, kiungo wa England na Chelsea, Ruben Loftus-Cheek (24), na Ross Barkley (26), lakini watalazimika kuchagua nyota mmoja kutokana na kanuni zilizowekwa za Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### ARSENAL YAMFUATA COUTINHO

ARSENAL imefufua uamuzi wake wa kuwania saini ya kiungo mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Sport - in Spanish)***

### FOFANA KUIKAMUA WEST

WEST Ham imewasilisha ofa ya pauni milioni 33 kwa ajili ya kumnasa beki wa kati wa Saint-Etienne Mfaransa, Wesley Fofana (19), ambaye ameivutia klabu ya Leicester City. ***(Sky Sports)***

### WILSON KUTUA BURNLEY

BURNLEY iko katika mazungumzo na Liverpool ili kunasa saini ya winga wa Timu ya Taifa ya Wales, Harry Wilson, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Independent)***

### HOEDT KUREJEA LAZIO

LAZIO imefikia katika makubaliano na Southampton ili kumrejesha beki Mholanzi, Wesley Hoedt (26), kwa mkopo katika klabu hiyo ya nchini Italia. ***(Sky Sport Italia - in Italian)***

### BARCA, BAYERN VITANI

BARCELONA na Bayern Munich wamewasilisha ofa ya kuwania saini ya beki wa kulia wa Ajax na Timu ya Taifa ya Marekani, Sergino Dest, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Marca)***

## New Generation yanukia ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya New Generation imerudi kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Wanawake, baada ya jana kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya timu ya Jumbi.

Kwa matokeo hayo, sasa New Generation inahitaji ushindi ama sare yoyote katika mechi yake ya mwisho dhidi ya Women's Fighter itakayopigwa keshokutwa, Jumamosi ili kutawazwa mabingwa wa ligi hiyo inayoshirikisha timu nne.

Katika msimamo wa ligi hiyo, New Generation ipo kileleni ikiwa na alama sita sawa na Women's Fighter wanayoizidi kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kwenye mechi hiyo ya juzi iliopigwa majira ya saa kumi alasiri katika Uwanja wa Mau B, New Generation, iliandika mabao mawili katika kipindi cha kwanza kupitia kwa wachezaji wake Hawa Farahm dakika ya 30, huku la pili likipachikwa nyavuni dakika ya 43 na nahodha wa timu hiyo, Riziki Abubakar.

Kipindi cha pili kilianza kwa timu ya Jumbi kujitahidi kuimarisha ulinzi langoni mwake, lakini dakika ya 89 New Generation waliandika bao la tatu kupitia kwa Warda Abdulhakim.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kumalizika mechi hiyo, nahodha wa New Generation, Riziki alisema licha ya kupata ushindi huo, lakini mchezo ulikuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao wana wachezaji wazuri na wanaojituma.

Alisema baada ya ushindi huo, akili yao sasa wanaielekeza katika mechi ijayo dhidi ya Women's Fighter itakaopigwa Jumamosi, ambayo itatoa mshindi.

## Kagera Sugar FC kuwakabili vinara

**Na Adam Nyangasa,** TUDARCo

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo kwa Kagera Sugar kuwakaribisha vinara wa ligi hiyo, KMC FC katika mechi itakayochezwa katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, alisema jana kikosi chao kiliwasili salama Bukoba na kiko tayari kwa mchezo huo wa raundi ya nne.

Mwagala alisema wamejipanga kuendeleza kasi ya ushindi na wanaamini wataibuka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Tumewasili salama mkoani Kagera tukitokea mkoani Shinyanga tulipoweka kambi maalumu ya kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu dhidi ya Kagera Sugar, tunajua kila timu iko vizuri, lakini sisi tumejipanga kutimiza malengo yetu," Mwagala alisema.

Aliongeza kikosi chao kilitarajia kufanya mazoezi ya mwisho jana jioni na hakuna majeruhi katika timu yao.

Mechi nyingine ya ligi hiyo inayotarajiwa kuchezwa leo ni kati ya Mbeya City dhidi ya Namungo FC katika Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

# MANARA AIHOFIA AZAM MBIO ZA UBINGWA BARA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wameitaja Azam FC kuwa ni timu pekee wanayoihofia kwenye mbio za kuwania taji hilo msimu huu.

**Azam FC imeshinda mechi zake tatu ilizocheza na kufikisha pointi tisa sawa na KMC FC, lakini klabu hiyo ya Chamazi haijaruhusu nyavu zake kutikiswa.**

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema Azam FC wana kikosi kizuri na wamejiandaa kuonyesha ushindani katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Manara (pichani) alisema Azam imesajili wachezaji wenye uwezo mzuri ambao unawasaidia kuamua matokeo.



"Nafurahi kuona msimu huu klabu nyingi zimesajili vizuri sana, tena wachezaji wenye uwezo. Hata KMC wamesajili vizuri sana, wanacheza soka zuri, wanapambana sana, lakini msimu huu naihofia zaidi Azam FC kwenye kinyang'anyiro cha kugombea ubingwa kutokana na usajili wao," alisema Manara.

Alimtaja mshambuliaji Prince Dube tayari ameshaonyesha uwezo wake katika kipindi kifupi kabla ya timu kupata mfumo na muunganiko mzuri.

Alisema kinachowabeba zaidi Simba ni kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa, ndiyo maana hata msimu uliopita walichukua ubingwa wakiziacha timu nyingine kwa idadi kubwa ya pointi.

"Simba tuna kikosi kipana na kila mchezaji ana uwezo mkubwa binafsi na wa kuamua mechi tangu msimu uliopita, kwa hiyo naona hata msimu huu tuna asilimia kubwa ya kuchukua ubingwa, ila Azam itatupa wakati mgumu sana msimu huu, ina wachezaji wa kweli ambao wana uwezo wa kupambana wenyewe na kuipa timu ushindi pale kila kitu kinapokataa uwanjani," Manara alisema.

KMC ndio vinara wa ligi hiyo kutokana na kuwa na idadi nzuri ya mabao ya kufunga ikifuatiwa na Azam wakati Simba yenye pointi saba iko katika nafasi ya tatu.



Mwenyekiti wa Klabu ya gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luwongo, akizindua vyumba vya kubadilishia nguo vya wanawake vilivyotengenezwa na Benki ya NCBA katika viwanja vya Lugalo jijini, Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Biashara na Huduma za Kidigitali wa benki hiyo, Gift Shoko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ujenzi vituo vya TFF wanukia*

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia makubaliano na Kampuni ya Six kwa ajili ya kusimamia mradi wa ujenzi wa vituo viwili vya kuendeleza soka vilivyoko Kigamboni jijini, Dar es Salaam na Tanga.

Akizungunza na jijini jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema baada ya kufikia makubaliano hayo, wanatarajia kuwakabidhi rasmi miradi hiyo kwa ajili ya kuanza mchakato wa ujenzi ifikapo Oktoba Mosi, mwaka huu.

Karia alisema gharama za ujenzi kwa kituo cha Kigamboni ni Dola za Marekani milioni 2.78 wakati kile cha Tanga ni Dola za Marekani milioni 2.4.

Alisema mradi huo utakuwa na awamu mbili, na fedha zitakazotumika katika ujenzi huo zimetoka katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) huku wakitarajia kuchukua muda wa mwaka mmoja.

Wakati huo huo, Makamu wa Kwanza wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani, alisema shirikisho hilo limepokea msaada wa vifaa vya ulinzi na usalama kutoka katika Kampuni ya Abood, ambayo inashughulika na uuzaji wa bidhaa za matairi.

Nyamlani alisema kampuni hiyo pia italipia gharama za mkufunzi ambaye atatoa elimu kwa wafanyakazi wa Idara ya Usalama wa TFF ambao wanafanya kazi kwenye viwanja vya michezo.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Eric Shija, alitaja thamani ya vifaa hivyo ni Sh. milioni 44 na lengo la kuvitoa ni kuchangia maendeleo ya soka nchini.

# Michezo

Ijumaa Septemba 25, 2020

Nipashe




Mendy mambo mazuri Chelsea UKURASA 22



Mshambuliaji wa Arsenal, Nicolas Pepe (kushoto), akijaribu kumtoka beki wa Leicester City, Wes Morgan (aliyeanguka), katika mechi ya Kombe la Ligi iliyochezwa kwenye Uwanja wa King Power juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Mastraika Yanga kubadilika Jumapili

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Mserbia, Zlakto Krmpotic, amesema anaamini timu yake 'itavuna' mabao mengi katika mechi dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa keshokutwa kutokana na mazoezi mapya aliyowapa washambuliaji wake.

Safu ya washambuliaji ya Yanga inaoongozwa na Michael Sarpong, Yacouba Sogne na Mukoko Tonombe.

Kauli ya Zlatko imekufa baada ya kutofurahishwa na idadi ya mabao ambayo timu yake imefunga katika mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo wamecheza.

Zlatko alisema amewapa washambuliaji wake majukumu ya kuhakikisha wanatumia vizuri nafasi watakazozitengeneza na kuongeza umakini wakati wote wa mchezo huo.

Kocha huyo alisema ili wapate ushindi, mechi dhidi ya Mtibwa Sugar ameigawa kwa awamu tatu na kila awamu washambuliaji wake watatakiwa kufuata maelekezo aliyotoa. Alisema ligi hiyo ina ushindani na ili kuwa kwenye nafasi salama ni lazima timu ipate ushindi na vilevile idadi nzuri ya mabao.

"Tumepata matokeo ya ushindi wa bao moja katika mechi zilizopita, ni mazuri kwetu kwa kuwa yanatusaidia kufikia malengo japo bado hatujafikia kwenye ubora ambao kila mmoja wetu angependa kuuona tukicheza, hasa kwenye kufunga idadi kubwa ya mabao," alisema Zlakto.

Alisema licha ya kila timu kuingia na mbinu zake, amewaandaa wachezaji wake kupambana na vile vile kuwaheshimu wapinzani wao.

"Kila mshambuliaji anatakiwa kutambua majukumu yake, wanatakiwa kuwa makini na nafasi wanazopata, ukitumia vyema nafasi unazotengeneza, basi tutafunga mabao ya kutosha, ni wazi tunatengeneza nafasi nyingi lakini zinapotea," Zlakto alisema.

Yanga yenye pointi saba, iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa nyuma ya vinara KMC, Azam FC, Simba na Dodoma Jiji FC.

# Rais CAF aikubali Simba

## ●●● Awatabiria makubwa msimu huu, huku Sven akiwaondoa hofu kutokana na Fraga...

**Somoe Ng'itu na Faustine Feliciane**

WAKATI Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad, akiwatakia Simba mafanikio, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, amewaondoa hofu mashabiki wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na kukosekana kwa kiungo, Gerson Fraga.

**Ahmad alimpongeza Ofisa Mtendaji mpya wa Simba, Barbara Gonzalez, kwa kuteulia kwenye nafasi hiyo na kumweleza anatakiwa afanye vizuri kwa ajili ya kutimiza malengo ya klabu hiyo.**

Rais huyo alimtaka Barbara kufanya vyema majukumu yake na 'kuwanyamazisha' wale waliobeza kutokana na jinsia yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Barbara, ambaye alitembelea ofisi za CAF zilizoko jijini, Cairo nchini Misri alisema anaahidi atafanya vyema na kuipeleka Simba kule ambapo mashabiki na wanachama wake wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu.

"Namshukuru Rais Ahmad na CAF kwa mapokezi mazuri, lakini ninaahidi kufanya kazi kwa bidii ili kusaidia kukuza soka la Afrika, nitayafanyia kazi mambo yote muhimu aliyonieleza yeye na viongozi wengine niliokutana nao," Barbara alisema.

Alisema pia hatawaangusha Simba kwa nafasi waliyompa na kupitia yeye atafungua milango ya wanawake wengine kuaminiwa kwenye uongozi wa soka.

"Ameniambia hii ni nafasi ya kuonyesha ninaimudu kazi hii na kupitia mimi itakuwa ni moja ya njia ya kuhamasisha wanawake wengine kushika nafasi za juu za uongozi wa soka," aliongeza ofisa huyo ambaye yuko katika ziara ya kujifunza kupitia klabu nyingine za Afrika zilizopiga hatua.

Ofisa huyo ambaye ameambatana na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mulamu Nghambi, pia alikutana na Katibu Mkuu wa CAF, Abdelmounaïm Bah pamoja na Makamu Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Anthony Baffoe.

Sven alisema ni pigo kumkosa Fraga ambaye aliumia katika mechi dhidi ya Biashara United, lakini wapo wachezaji wengine wenye uwezo wa kuziba nafasi yake.

"Ni mchezaji muhimu kwenye kikosi kama walivyowachezaji wengine, kuumia kwake ni pigo ingawa wapo wachezaji wanaoweza kucheza nafasi yake kwa ufanisi, bado sijapata taarifa ya mwisho ya madaktari ingawa nasoma kwenye baadhi ya vyombo vya habari kuwa atakuwa nje kwa mwezi mmoja, tunasubiri ripoti ya mwisho ya madaktari," alisema Sven.

Meneja wa timu hiyo Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kinaendelea vyema na mazoezi kuelekea mchezo wao dhidi ya Gwambina FC ambao pia unatarajiwa kuwa na ushindani.

"Ukimwondoa Fraga, wachezaji wengine wapo vizuri na wanaendelea na programu ya mwalimu kuelekea kwenye mchezo wetu na Gwambina," Rweyemamu alisema.

Mshauri wa Gwambina, Mwinyi Zahera, aliliambia gazeti hili kikosi chao kiko kamili kuwavaa Simba na wamejiandaa kuwashangaza mabingwa hao watetezi.

Zahera alisema licha ya kupoteza michezo iliyopita, lolote linaweza kutokea katika mechi ya kesho kwa sababu mpira wa miguu una matokeo ya kushangaza.

Taarifa za awali zinasema Fraga atakuwa nje kwa muda wa wiki tatu, hivyo atakosa mechi zinazofuata dhidi ya Gwambina, Mbeya City na Tanzania Prisons na watani zao, Yanga utakaochezwa Oktoba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >